LUGHA YA Kifaransa ULIMWENGUNI

Muhtasari 2022

toleo la 2022

Gallimard / Jumuiya ya kimataifa la Wanazungumzaji wa Kifaransa (Francophonie)

YALIYOMO

Dibaji

Utangulizi 4

SEHEMU 1
Uwepo na matumizi ya lugha ya Kifaransa ulimwenguni

- Hesabu na msambao wa kijiografia wa wazungumzaji wa Kifaransa 6
- Mtazamo wa Kifaransa wenye vitovu anuwai 10
- Lugha ya Kifaransa na wingilugha katika mashirika ya kimataifa 13

SEHEMU 2
Sera za lugha na ufundishaji wa Kifaransa ulimwenguni

- Kifaransa kama lugha ya elimu 20
- Kifaransa kama lugha ya kigeni 21

SEHEMU 3
Lugha ya Kifaransa, utamaduni na ulimwengu wa kidijitali

- Nafasi ya Kifaransa mtandaoni 26
- Maudhui ya utamaduni wa Kifaransa mtandaoni: thamani na changamoto za kugunduliwa 28
- Vitabu na waandishi ambao ni wazungumzaji wa Kifaransa 31

DIBAJI

Ripoti ifuatayo sio maelezo ya hali ya lugha ya Kifaransa ila ni wasilisho, muhtasari wa msambao wa lugha ya Kifaransa ulimwenguni. Inaanza kwa utambuzi ufuatao: "Tunazaliwa tukiwa na utambulisho mdogo wa Kifaransa, lakini tunazidi kuuimarisha"

Jumuiya ya wazungumzaji wa Kifaransa, kama ripoti inavyoeleza, ni mategemeo ya baadaye, mabadiliko, vitovu anuwai. Kwa kifupi, inaakisi vipengele anuwai vya ulimwengu.

Jumuiya ya wazungumzaji wa Kifaransa inawakilisha mategemeo ya kesho, kwa kuwa inapata nguvu kutokana na demografia ya bara la Afrika ambalo, kama Jumuiya ya wazungumzaji wa Kifaransa, inaelekea kwa vijana wake. Lugha ya Kifaransa hivyo basi ni lugha ya Afrika kuliko ilivyowahi kuwa hapo mbeleni, katika shule, uzalishaji wa fasihi, uendeshaji wa utafiti na hata wa fikra zake. Inaonyesha pia jinsi ya kuwa lugha ya kawaida ya mitaa yake, sokoni, katika majiji yanayozidi kukua kwa kasi.

Ulimwengu unaozungumza Kifaransa unakumbatia, kila mara, mabadiliko na tofauti ambazo zinazidi kutokea katika wingi wa tamaduni ambazo zinajumuishwa katika lugha hii wanayoshiriki. Hivyo basi, ni sehemu ya mviringo hai ambao tunaweza kusema "kitovu chake ni popote na mzingo wake haupo popote" kwa kufafanua taswira ya enzi ya kati.

Wingi wa maumbo na wingi wa vitovu, Jumuiya ya wazungumzaji wa Kifaransa ni sawa na wingi wa ulimwengu. Msingi wake ni kwamba wingi wa ulimwengu sio tu ukweli ila ni thamani ambayo sharti itoe mwelekeo. Jumuiya ya wazungumzaji wa Kifaransa hivyo basi ni ukuzaji endelevu wa wingi wa kiisimu na maadili yake katika ulimwengu na ndani mwake. Miongoni mwake, kwanza ni uwezo wa kufikiri kutoka lugha moja hadi nyingine, ambao pia ni uwezo wa kuigatua na kuifungua.

Hii ndio maana ripoti hii inasisitiza kuhusu ya "hatari ya umojalugha" kwa jumla, katika taasisi na hasa mahusiano ya kimataifa Si suala la kutisha au kujilazimishia lugha ambayo ingekuwa "bia" zaidi kuliko nyingine, lakini tena ni kuelewa kwamba katika ulimwengu wa tamaduni na nahau anuwai, ambazo ni nyingi kadri walivyo wanadamu, ipo mwishoni mwa mtagusano na lugha, mazungumzo yao ambayo yanaweza kuwa magumu, ya kuweka mpangilio katika uhusiano ambao kwa hakika haukosi kutokuelewana, ambayo hupatikana kuwa ya kawaida, ubia ambao ni muhimu kufanikiwa kwa pamoja. Ambayo yanaweza kuwa kwa mujibu wa mwanafalsa Maurice Merleau-Ponty, "pembeni" au "mlalo" bali sio "mning'inio"

Kutokana na wingilugha wa (wingi)pembeni, Jumuiya ya wazungumzaji wa Kifaransa ndio ishara na ufunuo.

Souleymane Bachir Diagne
Chuo kikuu cha Columbia

UTANGULIZI

Toleo hili la tano la *Lugha ya Kifaransa Ulimwenguni* linatuweka katikati ya Jamii tofauti zinazotumia Kifaransa ambazo zimezaliwa na kunawiri kadri lugha ya Kifaransa ilivyosambaa katika karne kadhaa. Lugha ya Kifaransa ikiwa na wazungumzaji milioni 321 ndiyo lugha ya 5 inayozungumzwa na watu wengi zaidi duniani (baada ya Kiingereza, kichina, Kihindi na kihispania)..

Kupitia msururu wa tafiti na uchanganuzi unaojikita kwa utafiti wa kiakademia, uhifadhi na uchanganuzi wa kitakwimu wa maendeleo ya kiisimu na kidemografia, mahojiano na ushuhuda, kitabu hiki kinatoa maelezo ya uwepo na matumizi ya Kifaransa katika miktadha anuwai ya kiisimujamii ambamo inakulia.

Imejazwa na ukweli kwamba wengi wa wazungumzaji wa Kifaransa na watoto wanaojifunza Kifaransa kwa mara ya kwanza wanaishi katika bara la Afrika.

Ili kuelewa hali hii, tunaombwa kutalii "ulimwengu wa wazungumzaji wa Kifaransa" katika sehemu ya kwanza ya kitabu hiki, ambayo inaeleza idadi na msamabo wa wazungumzaji wa Kifaransa ulimwenguni, lakini muhimu zaidi inaeleza uhalisia wa matumizi na viwango vya kujitwaliwa kwa lugha hii ambako mamilioni ya wazungumzaji hutumia, kubadilisha na kurutubisha kila siku katika mtagusano na uhalisia mwingine na lugha zingine. Uwasilishaji wa matokeo ya utafiti wa mwaka mzima katika nchi kumi kwenye eneo la kusini mwa jangwa la Sahara na Bahari Hindi unatuwezesha kushughulikia suala la aina za Kifaransa kwa kina na bila miiko.
Miongoni mwa thamani inayohusishwa na hali ya kilimwengu ya lugha ya Kifaransa na uanuwai wa miktadha yake ya matumizi, tunajikita katika kutathmini suala la wingilugha katika mashirika ya kimataifa. Kwa njia ya kipekee, tumeangazia athari ya mfumo wa "Tazama, tahadhari, hatua" ambao ulianzishwa mnamo 2020 na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya wazungumzaji wa Kifaransa, Bi Louise Mushikiwabo, ambaye alieleza katika mahojiano tuliyoendesha kwamba, "Wingilugha, ambao ni kigezo muhimu cha wingi wa pembe, ni mali ya pamoja na thamani ya kutetewa".

Sehemu ya pili ya kitabu hiki ni dafina ya taarifa sahihi kuhusu hali ya ujifunzaji wa Kifaransa katika takriban nchi 160. Kupima mabadiliko ya kilimwengu na kuwasilisha maendeleo na changamoto, maandishi ya watu binafsi yanayolenga kila himaya yanakamilishwa na uchanganuzi wa kina zaidi wa nyenzo ambao zinapendelea wingi wa lugha katika mifumo ya elimu. Idha, ni nafasi ya kueleza shughuli mbalimbali zinazofadhiliwa na Jumuiya ya wazungumzaji wa Kifaransa kusaidia zaidi ya **wanafunzi milioni 93** ambao wanatumia Kifaransa kama mojawapo ya lugha zao za elimu.
Kama lugha ya kigeni, Kifaransa ndio lugha ya pili watu wanajifunza ulimwenguni kwa zaidi ya watu **milioni 50**. Kukuza manufaa ya mafunzo ya Kifaransa kwa ajili ya matumizi ya kitaaluma kunawezesha kukiuka taswira ya kimapokeo ya lugha ya kiakademia au ya kiusomi na kuelekea kwa uamilifu ambao unaafiki upataji ajira, na uhamaji wa kitaaluma na wa wanafunzi. Tutagundua vilevile kwamba uhitaji wa Kifaransa ni muhimu na kwamba idadi ya wanafunzi wake inakuwa kwa kiwango kikubwa katika baadhi ya maeneo ya ulimwengu (Afrika, Amerika, Asia), hata kama upunguaji unaoshuhudiwa Ulaya unazalisha kutuama kwa kilimwengu.

Sehemu ya tatu inaanza kwa michoro inayoonyesha ya uwepo wa Kifaransa mtandaoni, jambo linalothibitisha **nafasi yake ya 4** (baada ya Kiingereza, kihispania na kiarabu), huku ikipendekeza mwelekeo asilia unaoangazia dhana ya "utandawazi wa lugha mtandaoni" ambao unaonyesha kiwango ambapo Kiingereza na Kifaransa zimejitenga na lugha nyingine.

Kisha tunatoa tahakiki ya suala jipya la "Ugunduzi" wa maudhui ya kitamaduni mtandaoni, ambayo inathibitisha - iwapo kweli - umuhimu wa masuala yanayohusiana na mpito wa kidijitali na maswali yanayoibuliwa na "uwekaji kwenye majukwaa" wa sekta za kitamaduni, hasa sekta ya maonoskizi na ya muziki. Kwa wakati huo huo, kwa kuripoti kuhusu Kongamano la kwanza la Ulimwengu la waandishi wanaozungumza Kifaransa lililofanyika mnamo 2021, na kwenye Mkutano Mkuu wa vitabu vya lugha ya Kifaransa ulimwenguni, tunajikumbusha kiwango ambacho vitabu vya Kifaransa na nafasi za kusoma hudhihirisha ukwasi wa ulimwengu wa kitamaduni na tukosefu wa usawa ambao ungali unahitaji kurekebishwa.

Alexandre Wolff
kiongozi wa French Language Observatory

SEHEMU YA 1

UWEPO NA MATUMIZI YA LUGHA YA KIFARANSA ULIMWENGUNI

Ongezeko la idadi ya wazungumzaji wa Kifaransa barani Afrika limekuwa thabiti kwa miaka kadhaa, na msambao wa wazungumzaji wa Kifaransa umebadilika pakubwa, kama yalivyo matumizi ya lugha hii katika miktadha ya wingilugha ambayo inapatikana katika bara la Afrika. Mbinu za kupata lugha ya Kifaransa pakubwa kupitia kwa mifumo rasmi ya mafunzo (lakini sio njia hii pekee), matumizi ya Kifaransa, huenda kwa nguvu kwa mujibu wa nchi zinazohusika, yanaongezwa kwa lugha moja au zaidi katika miktadha yenye urasmi mdogo, kwa mfano nje ya mazingira ya shule au taasisi rasmi. Isitoshe, wazungumzaji hawa wapya, ambao kwao Kifaransa sio lugha yao ya kwanza, katika hali nyingi, huisharabu kwa msingi wa stadi nyingine za kiisimu. Hali hii huongeza nafasi za mwingiliano baina ya Kifaransa na lugha za taifa, matokeo ya mtagusano huu huwa na sura tofauti: uundaji wa maneno mapya, uhamishaji katika Kifaransa wa misemo au maumbo kutoka lugha nyingine, kuibuka kwa lugha ambazo ni tofauti na Kifaransa sanifu. Kama anavyosema Richard Marcoux, mkurugenzi wa ODSEF[1], "Tunazaliwa tukiwa na utambulisho mdogo wa Kifaransa, lakini tunazidi kuuimarisha"

HESABU NA MSAMBAO WA KIJIOGRAFIA WA WAZUNGUMZAJI WA KIFARANSA

Kukiwa na takriban **wazungumzaji milioni 321 wa Kifaransa**[2] ulimwenguni mnamo 2022, lugha ya Kifaransa ingali katika kundi la lugha 5 zilizo na wazungumzaji wengi zaidi ulimwenguni (baada ya Kiingereza, kichina, Kihindi na kihispania[3]). Katika miaka minne, watu milioni 21 zaidi wanazungumza Kifaransa, ambalo ni ongezeko la aslimia 7% tangu mwaka wa 2018. Ukuaji ulioshuhudiwa katika miaka kadhaa sasa unazidi kuendelea kwa kasi nzuri, ingawa kasi hii imepungua kidogo. Kwa kweli, kwa vigezo sawa, idadi ya wazungumzaji wa Kifaransa iliongezeka kwa karibu asilimia 10% baina ya mwaka wa 2014 na 2018.

Kama wasomaji wetu walivyopata kuzoea, maelezo yetu huzingatia miktadha tofauti ambamo Kifaransa kinashamiri. Kwa sababu za kimbinu na kiamali, na zinazoepuka kutozingatia ukweli, tumeamua kutofautisha baina ya maisha ya kila siku ya Jumuiya ya wazungumzaji wa Kifaransa (ndani ya sayari "Kuzaliwa na/au kuishi katika Kifaransa") na Jumuiya ya wazungumzaji wa Kifaransa ambayo inajieleza katika mazingira ambamo Kifaransa ni lugha ya kigeni kikamilifu (cf. graph "The Francophone galaxy in 2022"). Nchi 36[4] zinazohusika, kando na kuwa zina takriban asilimia 80% ya wazungumzaji wa Kifaransa ulimwenguni, hujumuisha kikundi muhimu kwa siku zijazo katika lugha ya Kifaransa. Kwa hakika, umuhimu wa mienendo inayohusishwa na ujifunzaji wa Kifaransa kama lugha ya kigeni hauwezi kupingwa na vipashio vyake vinaeleza mengi kuhusu uwezo wa lugha ya Kifaransa kudumisha mvuto na umuhimu katika ulimwengu ambapo wingi lugha unaendelea. Ingawa hivyo, takwimu na tafiti ambazo tumekuwa tukikusanya kwa zaidi ya miaka 10 zinaonyesha kwamba, mustakabali wa lugha ya Kifaransa unaamuliwa katika bara la Afrika.



"Dunia" ya wazungumzaji wa lugha ya Kifaransa 2022

Kwa kweli, sio tu kwamba ukuaji wa idadi ya wazungumzaji wa Kifaransa kwenye sayari "Waliozaliwa na/au wanaoishi na Kifaransa" uko juu kidogo kuliko ule uliorekodiwa kwa ulimwengu kwa ujumla (pointi +1[5]), bali pia unawakilisha asilimia 95% ya ongezeko lililoshuhudiwa. Hivyo basi, zaidi ya "wazungumzaji wapya wa Kifaransa" milioni 19 wanaishi katika eneo hili, ambalo sehemu kubwa ipo Afrika.



Mgawanyo wa wazungumzaji wa lugha ya Kifaransa kila siku (2022)

Kwa kupata alama 2.5 za asilimia ikilinganishwa na 2018, bara la Afrika linathibitisha nafasi yake muhimu katika Francophonie ya kila siku na masuala yanayoitofautisha na maeneo mengine.

Itasaidia mahitimisho yetu kidogo, tunaona kwamba suala hili la kiafrika pakubwa ni kutokana na nchi za kusini mwa Sahara zinazowakilisha zaidi ya asilimia 80% ya ukuaji wa wazungumzaji wa Kifaransa katika eneo hili. Katika nchi hizi, isipokuwa katika nchi chache, viwango vya ukuaji kwa kweli viko juu zaidi ikilinganishwa na maeneno mengine. Ingawa idadi ya wazungumzaji wanaozungumza Kifaransa kila siku iliongezeka kwa asilimia 8% baina ya 2018 na 2022, idadi hii iliongezeka kwa zaidi ya asilimia 15% katika eneo la Kusini mwa Sahara na Bara Hindi (SS-JO).Kutokana na maendeleo haya chanya, masuala mawili yanapaswa kutambuliwa: ongezeko kila mahali liko chini kidogo kuliko ilivyokuwa baina ya 2014 na 2018 na yanabainisha tofauti dhahiri baina ya nchi.



Wazungumzaji wa lugha ya Kifaransa kila siku – Ongezeko kati ya 2018 na 2022

■ Je, ukuaji unapunguza kasi?

Kwa kila nchi, ni muhimu kutambua kwanza kwamba, maoni yoyote tutakayowasilisha hapa chini, ongezeko la idadi ya wazungumzaji wa Kifaransa katika eneo la Kusini mwa Sahara na Bahari Hindi angalau ni sawa na idadi ya jumla kwa kipindi sawa.

Ingawa hivyo, ikiwa tutachukua mtazamo wa kilimwengu, tutaona kwamba mabara yote katika sayare "waliozaliwa na/au kuishi katika Kifaransa" hawaongezi idadi ya wazungumzaji wa Kifaransa. Ukuaji ungali chini ikilinganishwa na ukuaji uliorekodiwa katika makadirio yetu yaliyopita. Tofauti ni asilimia 1% katika Ulaya na Oceania, alama 2 katika Amerika na katika eneo Kusini mwa Sahara na Bahari hindi, lakini alama 10 katika Afrika Kaskazini na Mashariki ya Kati.

Kiashiria ambacho pengine hakiathiriwi sana na hesabu tunayofanya kila miaka minne - na bila shaka ambacho ni muhimu zaidi wakati tunataka kuchukua muda kudhukuru swali hili kwa kipindi kirefu - kinapatikana kwenye mabadiliko ambayo yametokea katika asilimia za watu wanaochukuliwa kuwa wazungumzaji wa Kifaransa[6] katika kile mojawapo ya nchi katika sayare "aliyezaliwa na/au kuishi katika Kifaransa")

Kwa hivyo, hakuna nchi katika eneo la Afrika ambayo imeshuhudia mabadiliko makubwa katika asilimia ya watu ambao ni wazungumzaji wa Kifaransa ikilinganishwa na jumla ya watu. Tangu 2010, tunapata nchi zile zile katika hali sawa, sanasana chini ya asilimi 50% isipokuwa katika nchi 5 au 6 ambazo tayari zimepita upeo huu au ziko karibu sana. Hali hii inaweza kuchukuliwa kama dalili hafifu, zikigubika hali ya kutia moto kuliko iliyotumiwa katika utabiri (tazama Ukurasa wa 10) uliofanywa na washiriki wetu katika Chuo kikuu cha Laval (Demographic and Statistical Observatory of the Francophone Area, ODSEF).

[1]Kutoka, Demographic and Statistical Observatory of the French-speaking world of Laval University in Quebec.

[2]Kwa taarifa kuhusu hesabu, tazama maelezo ya utafiti Richard MARCOUX, Laurent RICHARD na Alexandre WOLFF. Estimation of Francophone populations in the world in 2022. Sources and methodological approaches. Kutoka Québec, 2022, Demographic and Statistical Observatory of the French-speaking world of Laval University (ODSEF. Voir QRcode.

[3]Makadirio ya idadi ya wasenaji wa lugha nyingine yalitokana na kitabu cha Ethnologue, Languages of the World. 23rd edition, 2020 cited by Wikipedia.

[4]Algeria, Andorra, Ubelgiji (ikiwemo shirikisho la Wallonia-Brussels), Benin, Burkina Faso, Burundi, Cameroon, Canada (ikiwemo Canada-New Brunswick, Canada-Ontario and Canada-Quebec), Comoros, Congo, DRC, Côte d'Ivoire, Djibouti, France (na himaya zake ughaibuni), Gabon, Guinea, Equatorial Guinea, Haiti, Lebanon, Luxembourg, Madagascar, Mali, Mauritania, Mauritius, Monaco, Morocco, Niger, Central African Rep., Rwanda, Senegal, Seychelles, Switzerland, Chad, Togo, Tunisia, Vanuatu.

[5]Hii kwa kweli iko juu kidogo, lakini marekebisho ya kushuka (ikilinganishwa na 2018) ya jumla ya wakazi wa baadhi ya maeneo ambapo wazungumzaji wa Kifaransa wana uzito wa zaidi ya asilimia 80% (Shirikisho la Wallonia-Brussels, Guadeloupe, Martinique, French Polinesia na Wallis & Futuna) kihisabati yaliipunguzia kasi.

[6]Hapa tena itakuwa hatari kuwasilisha asilimia za mabadiliko kwa kila nchi, baina ya 2010 na 2022 kwa mfano, bila kuzidisha tahadhari kuhusu mabadiliko katika vyanzo vilivyotumiwa na maelezo marefu ya kiufundi kuhusu athari za miundo ya kidemografia. Hivyo basi tunachagua kuwasilisha mtazamo wa jumla.

MSONGAMANO WA WAZUNGUMZAJI WA KIFARANSA DUNIANI KATIKA MWAKA WA 2022



Idadi ya wazungumzaji wa Kifaransa duniani – Utabiri wa ODSEF



Tunajua kwamba mabadiliko madogo huenda yasiarifu hali kamili, hata hivyo tunatoa mapendekezo ya jumla.

Katika hali ya kwanza, na bila kujali tahadharia za kimbinu zilizochukuliwa, inaelekea kuwa vigumu kuhitimisha kwamba nchi hizi zimezidi kukika mizizi yake ya Kifaransa. Lugha ya Kifaransa inadumisha uwepo wake, lakini haielekei kupanua nafasi yake. Ikiwa katika kipindi kirefu mgao wa wazungumzaji wa Kifaransa utakuwa kwa kiasi kinachobainika dhahiri, sharti tutambue kwamba inaelekea kuwa imfikia ukomo fulani, japo kwa haraka (katika takriban miaka ishirini) Kuanzia kwa msingi finyu, kwa sababu sharti ikumbukwe kwamba kipindi cha ukoloni kilichangia kidogo sana katika kusambaa kwa Kifaransa miongoi mwa watu, kiwango cha watu wanaozungumza Kifaransa kimeongezeka maradufu hasa kutokana na shule. Kutoana na maendeleo ya shule, Kifaransa kimezidi kuimarika japo kwa kasi ndogo. Hali hii inathibitisha tahadhari zilizotolewa mara kwa mara tangu 2010 kuhusu hali ambazo ni muhimu kwa siku zijazo za Jumuiya ya wazungumzaji wa Kifaransa barani Afrika.

Kwa kuhitimisha, inaelekea kwamba changamoto zinazohitaji kushughulikiwa katika msingi wa ubora wa elimu kwa Kifaransa ni za dharura kuliko ilivyokuwa awali. Kwa jinsi hii, matokeo ya hivi punde zaidi ya utafiti wa PASEC[7] katika nchi 14[8] ambazo ni wanachama wa Kongamano la Mawaziri wa Elimu ya Mataifa na Serikali za Jumuiya zinazozungumza Kifaransa (CONFEMEN) si ya kutia moyo sana. Kwa kweli, mwanzoni mwa mzunguko huu[9], zaidi ya asilimia 55% ya wanafunzi, kwa wastani, hawajafikia kiwango "toshelevu" katika lugha. Vivyo hivyo, kufikia mwishoni mwa mwaka wa kiakademia, zaidi ya nusu ua wanafunzi (aslimia 52.1%) ilikuwa chini ya kiwango "toshelevu" cha umilisi. Ripoti ya PASE2019 inatambua kwamba matokeo kwa wastani ni bora kuliko yale yaliyoshuhudiwa katika tathmini ya awali mnamo 2014, ingawa baadhi ya nchi zimeanza kutuama au hata kurudi nyuma.

Uhalisia wa kiisimujamii unaonyesha baadhi ya sifa sawa, hata hivyo aghalabu ni tofauti baina ya nchi moja na nyingine. Hali hii ni kweli hasa kwa **matumizi ya Kifaransa, ambayo yanatofautiana pakubwa, kutegemea mahali** palipotwaliwa na lugha ya kitaifa inayotumika na wengi (tazama grafu "Viwango vya Kifaransa" hapa chini), lakini pia kulingana na mienendo ya mjini.

MAONO YA VITOVU VYA KIFARANSA

Utafiti wa hivi punde zaidi wa Taasisi ya Kantar, ambao matokeo yake tulitumia, na ambao uliangazia miji katika nchi 15[10], uliendeshwa katika robo ya pili ya 2020 na robo ya kwanza ya 2021. Matokeo yanaonyesha ufahamu wenye maana lakini unaotofautiana wa Kifaransa katika nchi zote kwenye sampuli. Watu wengi walijitambulisha kuwa wazungumzaji wa Kifaransa: baina ya asilimai 57% (katika miji ya Senegal) hadi kufikia asilimia 90% (katika Miji ya Kongo), lakini umilisi halisi wa Kifaransa unazingatiwa na idadi ndogo ya watu. Kwa mujibu wa viashiria vilivyobainishwa na Kantar kueleza "Msemaji wa Kifaransa mwenye Umilisi" safu inasambaa kutoka asilimia 28% (mijini Burkina Faso) hadi asilimia 68% (mijini Algeria)

Kutoka kwa mtazamo wa mageuko, tunaweza kutambua uthabiti katika viwango vya wazungumzaji wa Kifaransa waliotambuliwa na wasailiwa. Kwa kuwa utafiti wa awalizaidi tulionao ni ule uliofanywa 2008, kiasi fulani cha usuli kinatusaidia kutoa mawazo fulani. Ikiwa nchi nyingi zinazohusika hazielekei kuwa zimeshuhudia mabadiliko yoyote muhimu, ama katika idadi ya watu wanaojitambulisha kama wazungumzaji wa Kifaransa au katika idadi ya watu wanaozingatiwa kuwa na "umilisi katika lugha ya Kifaransa", tunaweza kutambua hali mahususi.

[7]PASEC2019. Quality of Education Systems in Francophone Sub-Saharan Africa. Performance and teaching-learning environment in primary education. Voir QRcode.

[8]Benin, Burkina Faso, Burundi, Cameroon, Chad, Congo, Côte d'Ivoire, Jamhuri ya kidemokrasi ya Kongo, Gabon, Guinea, Madagascar, Niger, Senegal, na Togo.

[9]Tathmini zilijikita kwa elimu ya msingi pekee

[10]Morocco, Algeria, Tunisia, Mauritania, Central African Republic, Togo, Rwanda, Senegal, Cote d'Ivoire, Cameroon, DRC, Gabon, Mali, Burkina Faso, Congo.

Kuna idadi kubwa ya watu wanaozungumza Kifaransa katika kanda nzima hasa katikati mwa bara la Africa na nchi za Maghreb*



*Matokeo yanahusu miji mikuu au ya upili pekee katikamataifa yaliyotajwa.

Hivyo basi, wakaazi wa miji nchini Gabon na Morocco wanadhihirisha ongezeko la "umilisi wa Kifaransa" pamoja na ongezeko la idadi ya wazungumzaji wa Kifaransa. "Umilisi wa Kifaransa" ia umeongezeka pakubwa katika miji ya Ivory Coast, huku viwango vya wazungumzaji wa Kifaransa kwa jumla vikisalia vile vile. Miji nchini Mali na Tunisia pia inaonyesha ongezeko la idadi ya watu wanaojitambulisha kuwa wazungumzaji wa Kifaransa baina ya 2010/2011 na 2020/2021 (ongezeko la alama 17 na 18 mtawalia). Kwa upande mwingine, ingawa idadi ya jumla ya wazungumzaji wa Kifaransa katika miji nchini Jamhuri ya kidemokrasi ya Kongo ni thabiti, mgao wa wazungumzaji walio na umilisi bora katika lugha ya Kifaransa unashuka kwa alama 7 baina ya 2009 na 2020/2021. Miji ya Senegal inaonyesha ruwaza tofauti ambapo, idadi iliyothibitishwa ya wazungumzaji wa Kifaransa inasalia kuwa thabiti, lakini idadi ya jumla ya wazungumzaji wa Kifaransa ikipungua (kwa alama 5 baina ya 2009 na 2020/2021).

■ Ruwaza inayotawaliwa na vijana

Idadi kubwa ya wazungumzaji wa Kifaransa katika eneo la Kusini mwa Sahara na Afrika Kaskazini ni watu walio na umri baina ya miaka 15-24. Hii inadhihirisha uwezekano mkubwa wa ukuaji wa jumuiya inayozungumza Kifaransa. Kwa kweli, matokeo yanayonyesha kwamba vijana hawa ni wengi kuweza kukimanya Kifaransa ikilinganishwa na wazee wao. Isipokuwa Mali, Rwanda na Togo, na kwa kiasi kidogo Congo na Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo, mgao wa vijana wanaoishi mijini ambao wana umilisi katika Kifaransa uko juu zaidi ya vikundi vingine kiumri. Pengo baina ya makundi haya kwa wastani ni alama 6, lakini katika baadhi ya hali (katika nchi 4) pengo hili ni alama 10 au 20! Hii bila shaka ni thibitisho kuhusu siku zijazo kwa lugha ya Kifaransa, ambazo tumeshatambua katika tafiti nyingine zinazoonyesha matumizi zaidi ya Kifaransa miongoni mwa vizazi vya umri wa chini.

Zaidi ya umri wao mdogo, wazungumzaji wengi wa Kifaransa mijini ni watu ambao wamepata elimu ya msingi (angalau shule ya msingi, lakini sana sana elimu ya sekondari au juu zaidi) na wamo katika kategoria ya juu kiuchumi katika jamii. Hii inaashiria umuhimu wa shule, ufikiaji wake kwa kiasi fulani unat-

egemea viwango vya mapato, ambayo nayo yanahusishwa na hadhi ya mtu, na kwa jinsi hiyo mahusiano yake kijamii, mtagusano kitamaduni, na mazingira ya kitaaluma, yote yakiwa masuala ambayo yanachangia wingi na ubora wa matumizi ya Kifaransa.

■ Nafasi inayotambuliwa kwa Lugha ya Kifaransa

Mahusiano haya baina ya umilisi katika lugha ya Kifaransa na nafasi ambazo lugha hii inawasaidia wazungumzaji wake kupata yanaakisiwa vizuri katika majibu kuhusu umihimu wa lugha hii katika fani mbalimbali. Kwa hivyo, Kifaransa aghalabu kinatambuliwa kwa ajili ya uwezo wake wa:

- Kusaidia kupata ajira (baina ya asilimia 67% na 97% ya maoni)
- Elimu (baina ya asilimia 68% na 98%)
- Kupata taarifa (baina ya asilimia 49% na 98%)
- Kuendesha utafiti mtandaoni (baina ya asilimia 53% na 97%)
- Kufikia tamaduni nyingine (baina ya asilimia 55% na 96%)

■ Kifaransa kama lugha ya pili

Tathmini ya matumizi ya Kifaransa kwa kuzingatia muktadha imefanywa kupitia maswali yaliyoulizwa ili kuzigawa lugha zinazotumika nyumbani na kazini kwa kutofautisha ile ambayo matumizi yake yanatukia zaidi (lugha kuu) na lugha nyingine, kwa mpangilio wa umuhimu.

Kazini

Kifaransa kinatumika katika hali zote. kinabainika zaidi ("Lugha kuu") katika miji nchini Côte d'Ivoire, Cameroon, Congo, Gabon (ambapo Kifaransa ndiyo lugha ya pekee inayotajwa) na katika Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo. Katika nchi nyingine zote, isipokuwa nchini Burkina Faso (ambapo lugha za Mooré na Dioula zinatumika zaidi) na Rwanda (kinafuata kinyarwanda na Kiingereza), Kifaransa ndiyo lugha ya pili ambayo inatumika zaidi kazini katika miji.

Nyumbani

Matukio ya matumizi ya Kifaransa nyumbani yangali chini ikilinganishwa na ilivyo kazini - wakati mwingine hata kinatoweka, kama ilivyo katika miji nchini Senegal na Mauritania - lakini nafasi yake katika tabaka la lugha ingali thabiti. Kifaransa hata kinachukua nafasi ya kwanza katika maeneo ya mijini nchini Côte d'Ivoire, Cameroon, Congo na Gabon. Katika miji ya nchi mbalimbali, Kifaransa ni lugha ya pili katika matumizi: Algeria, Mali, Central African Republic, DRC na Togo. Mwisho, nchini Morocco, Tunisia na Rwanda, nafasi yake ni ya pembeni zaidi na inaweza kuefafanuliwa kuchukua nafasi ya pili au tatu "lugha nyingine" ambayo inaweza kutumiwa kwa mawasiliano katika familia, lakini inatumika.

Kwa muhtasari, matokeo ya tafiti yanaonyesha yafuatao :

→ wazungumzaji wote wa Kifaransa katika maeneno haya ni wanawingilugha na lugha yao ya kwanza muhali huwa ni Kifaransa ;
→ Upataji wa lugha ya Kifaransa unahitaji juhudi na ujuzi wake, bila kuzingatia umilisi kamili, unapatikana miongoni mwa sehemu ya jamii;
→ Hadhi ya urasmi wa Kifaransa na ubora wake kama lugha ya kufundishia ni mambo ambayo hayatoi hakikisho la usambazaji wa jumla, wala umilisi wake, au matumizi yake ;
→ Nafasi hii ya kipekee (bila kulinganisha na lugha nyingine za kigeni au lugha za kieneo au hata za kitaifa) inayochukuliwa na lugha hii inaifanya iweze kuitika Lugha ya kiafrika, inayomilikiwa na wazungumzaji wake ; na
→ Baadhi ya dalili za uthabiti wake na uwezekano wa kukua (wazungumzaji vijana, ushahidi wa matumizi nyumbani na katika shughuli za kiuchumi) zinahitaji umakini maalum.

■ Tofauti za kiisimu-jamii za Kifaransa

Swali lingine, kwenye makutano ya mbinu za upataji, matumizi na ufahamu wa Kifaransa na lugha nyingine, linahitaji mwelekeo wakina zaidi. Msomaji pia ataweza kunufaika kutokana na matokeo ya utafiti wa hivi karibuni ulioendeshwa katika nchi kumi barani Afrika[11], ukiangazia maoni yaliyotolewa kuhusu matumizi tofauti ya Kifaransa Mahojiano tuliyoendesha na Professor Bernard Cerquiglini, mwanaisimu na rais wa kamati ya kisayansi ya Kamusi ya wazungumzaji wa Kifaransa (DDF[12]), yanaonyesha kiwango ambacho suala hili limekuwa la shauku kubwa.

[11] Algeria, Benin, Cameroon, Chad, Côte d'Ivoire, Ghana, Lebanon, Morocco, Madagascar na DRC.
[12] Voir QRcode.

Uchunguzi wa lugha ya Kifaransa ulianzisha utafiti huu wa utalii[13] kuhusu suala la tofauti za kiisimu-jamii za Kifaransa, mtazamo wa wazungumzaji wake na matumizi yake, hasa katika uwanja wa elimu. Watafiti aidha walialikwa kutalii njia zinazowezekana za "usimamizi uliounganishwa" wa lugha ya Kifaransa, ambayo inadhukuriwa kuwa mali asili ya wazungumzaji wake wakote, iwe wanaishi Paris, Darak au kinshasa. Kwa mujibu wa tahakiki ya matini, hojaji, mahojiano na utazamaji wa moja kwa moja darasani, kazi ya watafiti imewezesha utambuzi wa mienendo michache.

Lugha ya Kifaransa inachukuliwa, na wazungumzaji ambao sio wazawa wa lugha hii, kimsingi kuwa nyenzo ya kiuamilifu, katika mahusiano yanayoongozwa na uamali na matumizi. Hali hii ni sawa kwa *lugha za kitaifa*, ambazo matumizi yake na maazimio yanayoambatana yanadhihirisha mwelekeo wa kupambana. Ni muhimu vilevile kutambua kwamba, licha ya kuwepo akilini mwa wazungumzaji, chanzo cha kihistoria na majilio ya lugha ya Kifaransa kwenye bara Afrika na katika Bahari Hindi (ukoloni), yanaibua hisia chazhe za chuki. Ingawa hali yake ya kulazimishwa, au hata "amrishwa" inaweza kutambuliwa, kutoridhishwa kunakoweza kuibuka kungeonyeshwa dhidi ya sera za kitaifa, jambo ambalo, miaka sitini baada ya uhuru, liinaonekana kuwa lenye mantiki. Hata hivyo, hii haimaanishi kwamba wananchi hawatambui masilahi ya nchi zinazotumia Kifaransa upande wa Kaskazini, na hasa kwa Ufaransa, kudumisha na kuzidisha uwepo wa lugha ya Kifaransa katika ngazi ya kimataifa. Ingawa hivyo, wanasisitiza zaidi uamilifu ambao umilisi wa lugha hii unawakilisha. Hatimaye, matumizi ya mara kwa mara ya Kifaransa, ambayo yanaonekana kuthibitishwa, hayapunguzi mazoea ya wingilugha ambayo bila shaka ni sifa ya miktadha ya jumuiya ya wazungumzaji wa Kifaransa ya Kusini.

Wake wa kusaidia na kuthamini wingilugha huku zikikuza umuhimu wa Kifaransa.

Suala la tofauti katika Kifaransa, haliwezi kukataliwa, hata hivyo tofauti hizi pia hazijadaiwa. Hatimaye, wazungumzaji wachache wanakiri matumizi yake, licha ya kutambua uwepo wake na matumizi kwa jumla. Mbali na matatizo wanayokumbana nayo katika kufafanua sura za kategoria hii ya lugha – pamoja na watafiti wanaochapisha kuhusu masuala haya – ni wazi kuwa kuna kusitasita kutoa madai. Hata hivyo, kauli kuzihusu, ikiwemo uzingatiwaji katika mchakato wa kujifunza, unadhihirisha hisia za haja ya kuelewa suala hili na ya "kutenga nafasi" kwa tofauti katika Kifaransa. Nafasi hii haipo katika shule, ingawa walimu wengi wanatoa kipaumbele kwa kile kinachojulikana kama Kifaransa "sanifu" darasani, huku kwa nadra wakirejelea aina tofauti za Kifaransa (pamoja na lugha za kitaifa) almradi zinasaidia katika kukuza maingiliano na upataji wa maarifa yanayosambazwa. Kwa wakati huo huo, wana shaka kuu kuhusu uhalali, na hasa umuhimu, kwa msingi wa matokeo, wa matumizi ya Kifaransa cha aina Tofauti kwa mafanikio ya wanafunzi.
Bila shaka hili ni suala linalopaswa kuzingatiwa ili kuwasaidia walimu, palipo na haja, kwa kutambua "desturi faafu" ambazo hazitachukuliwa kuwa "mwiko", almradi zinahakikisha ufundishaji bora...

[13] "Pratiques et représentations socio-langagières des français en Francophonie" (PRESLAF). Ripoti kamili na matokeo ya utafiti yanaweza kupatikana kupitia anwani ifuatayo. . Voir QRcode.

LUGHA YA KIFARANSA NA WINGILUGHA KATIKA MSAHIRIKA YA KIMATAIFA

■ Hatari ya umojalugha

Ripoti za mashirika ya kimataifa na machunzaji wa nje zinakubaliana katika kusikitikia matumizi ya lugha ambayo yanaelekea kukosa kuheshimu wingilugha. Ukosefu wa usawa unaripotiwa Kiingereza kikipendelewa huku lugha nyingine rasmi au za kufanyia kazi zikitelekezwa katika kazi ya mashirika haya yote, hasa katika mchakato wa kuajiri watu, mawasiliano ya nje na simu zinazohusu kandarasi au miradi.

Ripoti ya hivi punde zaidi ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa juu ya wingilugha inaangazia matatizo yanayojirudia kwa baadhi ya mipango ya kutekeleza wingilugha. Kiingereza kinasalia kuwa lugha inayopendelewa katika Umoja wa Mataifa katika ajira - asilimia 98.7% ya kazi zinazotangazwa huhitaji ujuzi wa Kiingereza, huku Kifaransa kikishuka kwa alama 1.2 tangu 2017 (kufikia asilimia 10.4%) - na katika mawasiliano ya ndani kwa ndani: Asilimai 98% ya yaliyomo kwenye mitandao ya ofisi zinazohusishwa na Ofisi kuu yanapatikana lwa Kiingereza (ongezeko la alama 23 tangu 2018), ikilinganishwa na asilimia 16% kwa Kifaransa.

Kitengo cha Pamoja cha Ukaguzi (JUI) cha mfumo wa Umoja wa Mataifa[14] katika ripoti yake ya hivi punde zaidi kinadokeza, ukosefu wa maendeleo na haja ya asasi za utawala kuchukua hatua ili kuhakikisha kwamba kuna usawa unaohitajika baina ya utekelezaji faafu wa wingilugha na ugawaji wa rasilimali zinazohitajika.

Katika Umoja wa Ulaya, hali si bora kwa wingilugha: ni baina ya asilimia 3.7% pekee (katika Kamisheni ya Ulaya) na asilimia 12% (Katika Bunge la Ulaya) ya nyaraka zinazozalishwa zinatolewa kwa Kifaransa kama lugha chanzi, idadi inayozidi kupungua katika miaka ishirini iliyopita,wakati mgao ulikuwa asilimia 34% (mnamo 1999).

Itakuwa jambo muhimu kukomesha mkondo huu kwa sababu, kwa mujibu wa tafiti, ni asilimia 25% pekee ya wananchi wa Ulaya ambao wanaweza kuelewa makala ya gazeti au taarifa ya maonoskizi kwa Kiingereza[15] na tangu Uingereza kujiondoa kwenye Muungano wa Ulaya, chini ya asilimia 1% ya wananchi katika mataifa ambayo ni wanachama wanatumia Kiingereza kama lugha ya mama...

Maoni yaliyotolewa kwa Umoja wa Mataifa na kwa Umoja wa Ulaya yanaelekea kufafana na yale ya mashirika ya kieneo au kimataifa kama inavyoonyeshwa kwenye nyaraka ya mwisho ya ufuatilizi kwa IOF's vade mecum of La Francophonie, ambayo pia inaguzia Umoja wa Afrika, Bunge la YUlaya na Baraza la Bara la Ulaya.

■ Kuelekea kwa mfumo unaofanya kazi wenye viambajengo vitatu: ufuatiliaji, tahadhari na hatua

Kwa kujitolea "kukabili kuzorota kwa lugha ya Kifaransa", Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazungumzaji wa Kifaransa, Bi Louise Mushikiwabo, ameanzisha tafakuri kubwa na wawakilishi wa Mataifa na serikali ndani ya kikundi kazi cha "lugha ya Kifaransa" ambayo ameanzisha na huongoza vikao mara kwa mara.

"Mfumo wa ufuatiliano, tahadhari na hatua unaopendela lugha ya Kifaransa na Wingilugha katika msahirika ya kimataifa", kwa msaada wa Nchi na serikali ambazo zinazungumza Kifaransa umeanzishwa ili kuwezesha ubadilishanaji wa taarifa, uratibu wa miakakti inayotumiwa pamoja na uhamasishaji wa mitandao inayozungumza Kifaransa. Mtandao wa vitovu vya kitaifa umeanzishwa kushiriki katika shughuli za ufuatiliaji na tahadhari kuhusu ukiukaji uliothibitishwa wa utaratibu wa lugha katika mashirika ya kimataifa.

Utetezi wa kisiasa na Uhamasishaji wa Nchi na Serikali

Kutoka makao yake makuu kule Paris na kupitia kwa wawakilishi wa nje[16], hasa wale wanaofanya kazi katika mashirika ya kimataifa, IOF imekuwa ikijihusisha katika utetezi katika ngazi mbalimbali, pamoja na kupitia kwa shughuli nyingi ikiwemo uratibu wa Francophone Ambassadors' Groups (GAF) na mitandao ya kimataifa ya watumishi wa umma. Katibu mkuu katika nafasi yake kila mara huendesha utetezi katika viwango vya juu zaidi na viongozi wa nchi na wa serikali, viongozi wa mashirika ya kimataifa na hata Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa

Kutokana na msaada wa Wawakilishi wa Nje wa IOF, mikutano kadhaa na juhudi zimefanikishwa kuimarisha jukumu la GAF na hatua zao kutetea wingilugha. IOF pia imewasaidia na jukwaa la kidijitali la kuwaleta pamoja katika mtandao wa kilimwengu kufikia mwanzoni mwa 2022.

■ Msaada wa IOF

Kushirikiana na mashirika ya kimataifa na kieneo (IROs)

Ushirikiano wa karibu wa IOF mashirika ya kimataifa na ya kieneo katika kushabikia wingilugha umeibua juhudi kama vile: uzinduzi wa Mei 2021 wa Msururu wa mafunzo ya kiufundi katika Kifaransa kwa maafisa wa umoja wa Afrika; maandalizi ya 2021 ya mtalaa katika mawasiliano ya kitaaluma na Kifaransa cha kisheria kwa Mahakama ya kimataifa ya Jinai ; Uchapishaji wa wito wa ilhamu mnamo 2021 uliolenga kuimarisha stadi katika lugha ya Kifaransa kwa watumishi wa umma na upatanisho wa kiisimu (miradi 9 iliyochaguliwa; mashirika 8 ya kieneo na kimataifa yalinufaika).

[14] Ripoti hii inajumuisha mahojiano ya kina na uchanganuzi wa kitakwimu na wa kithamano wa data iliyokusanywa kutoka kwa
matini, majibu ya hojaji na mahojiano (zaidi ya mahojiano 100 na wawakilishi wa asasi mbalimbali za Umoja wa Mataifa walio
Geneva, New York, Paris, ROma na Vienna na katika ofisi mbili za nyanjani: Brussels na Nicosia).

[15] Special Eurobarometer 386, 2012.

[16] Addis Ababa, Brussels, Geneva, na New York, pamoja na Antananarivo, Bucharest, Dakar, Hanoi, Libreville, Lomé, Port-auPrince, Quebec, Tunis, na hivi karibuni Beirut.

Mafunzo na uimarishaji wa uwezo

Ili kuimarisha uwezo wa Nchi au taasisi za kitaifa za mafunzo katika kujeleza na kutekeleza mipango ya mafunzo katika Kifaransa kwa ajili ya (watakaokuwa) wahumudu wa umma na wanadiplomasia, IOF inatumia mipango ambayo inalenga kuongeza idadi ya wasimamizi na watalamu katika tawala zilizolegwa walio na kiwango toshelevu cha Kifaransa kuweza kujieleza kwa Kifaransa katika mazingira yao ya kitaaluma. Ndani ya mpangilio huu, serikali kumi na tisa za kitaifa au taasisi zimetia saini Makubaliano ya Ushirikiano (Mpango wa National Francophone na Mpango wa Francophone Establishment Initiatives - IFN na IFE) na IOF kwa kipindi baina ya 2019-2022. Zaidi ya wakala 1,200 - ambao angalau asilimai 70% miongoni mwa ni wanawake - wanapewa mafunzo kila mwaka.

Kutoa nyenzo na rasilimali

Mnamo 2020, IOF ilizidi kusaidia TV5MONDE katika kuzalisha vipindi 42 vya taarifa ("7 jours sur la planète"), mazoezi 1,080 ya kujifunza na karatasi 262 za elimu. Kwa mafunzo ya kujisimamia, kuna makusanyo fulani ambayo yamepata mafanikio makubwa, kama vile "Le français des relations internationales", yanayowalenga watu wanaojiandaa kwa ajili ya stashahada katika mahusiano ya kimataifa (DFP-RI) ya Baraza la Biashara na Viwanda la Paris-Île-de-France ,au "Objectif diplomatie", kwa utangulizi kwa Kifaransa cha Mahusiano ya kimataifa katika miktadha rasmi au isiyo rasmi. Mnamo Machi 2020, TV5MONDE ilizindua programu ya "Jifunze Kifaransa na TV5MONDE", ambayo inasheheni mazoezi 3000 kwenye apprendre.tv5monde.com.

Tangu 2017, IOF pia imeshirikiana na Hachette FLE kuchapisha *Objectif* diplomatie daraja la 1 toleo jipya, kitabu kinacholenga ujifunzaji wa Kifaransa kwa wanadiplomasia. Mnamo Desemba 2019, ofa hii iliimarishwa na kozi ya kidijitali ya mazoezi 150yanayojisahihisha na, kufikia mwishoni mwa 2021, *Objectif* diplomatie.labdarala la 1, nyenzo ya kidijitali inayopatikana bila malipo kwa walimu iliwekwa mtandaoni.

Sehemu maalum ya "amani na usalama"

Ili kuimarisha uwepo wa wazungumzaji wa Kifaransa katika Umoja wa Mataifa, PKO (inakadiriwa kuwa asilimia 27% kufikia Januari 2021, huku miradi mingi ikitekelezwa katika maeneo ambamo Kifaransa kinazungumzwa), IOF ilikuwa inachukua hatua, ambapo nyingi miongoni mwake zimezalisha matokeo yanayoonekana. Miongoni mwa juhudi hizi ni mradi wa IOF-UN-France Pilot wa kuimarisha lugha ya Kifaransa katika mfumo wa ukufunzi kwa wanajeshi wa MINUSMA[17] (Mei 2021 hadi sasa).

Dans le cadre d'un partenariat développé par l'OIF avec la Kama sehemu ya ushirikiano baina a IOF na kitengo cha Polisi cha Umoja wa Mataifa, kumekuwa na seminaa mbili za pamoja zilizopangwa tangu 2018 jijini Paris na Bamako, kwa msaada wa mtandao wa ukufunzi wa polisi wa Francopol kuimarisha ubora wa programu zinazowasilishwa na wazungumzaji wa Kifaransa. Ongezeko katika idadi ya maafisa wa polisi wanaozungumza Kifaransa imeshuhudiwa: kutoka asilimia 28% mnamo 2021 hadi asilimia 80% ya maafisa kufikia 2021

Mifano mingine ya ukufunzi kwa wazungumzaji wa Kifaransa inajumuisha: kozi ya kwanza ya ukufunzi kwa Kifaransa kwa viongozi wa mipango, ambao kufikia sasa umekuwa ukiendeshwa kwa Kiingereza; kozi ya kwanza ya Kifaransa kwa maafisa wa kike katika jeshi; na ukuzaji wa kozi ya ukufunzi katika lugha ya Kifaransa kwa washauri wa usawa wa kijinsia katika PKO.

Mafanikio mengine ambayo yameshuhudiwa ilikuwa mnamo 2021 kupitia uzinduzi wa Réseau d'expertise et de formation francophone pour les opérations de paix (REFFOP), ambao sasa umeinganishwa kwenye tovuti ya Boutros-Ghali Peacekeeping Observatory Mtandao huu unalenga kuimarisha ustadi katika Kifaransa na uwezekano wa shulle na vituo vya mafunzo ya kulinda alamani Afrika, Marekani, Bara la Ulaya na Kusini Mashariki mwa Asia. Rasilimali za ukufunzi wa kulinda amani kwa kifarasa zinapatika mtandaoni.

Kifaransa, lugha rasmi ya Michezo ya Olimpikina Olimpiki ya Walemavu

Kwa kila shindano, IOF inatoa wafanyakazi wanaozungumza Kifaransa kwa Kamati Andalizi ya Michezo ya Olimpiki[18] ambao ni watalamu wa tafsiri wanaotumwa

[17] United Nations Multidimensional Integrated Stabilization Mission in Mali

[18] Voir QRcode.

kwenye huduma za lugha na kwenye vyombo vya habari, ambao huchangia tafsiri na ufafanuzi wa yaliyomo kwa Kifaransa. Tangu 2004, mtu amewekwa na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya wazungumzaji wa Kifaransa kuhakikisha uzingatiaji wa kifungu cha 23 cha Mkataba wa Olimpiki[19]. Mpango wa Grand Témoin de la Francophonie katika mashindano ya 2020 umekabidhiwa Thierry Marx, Mpishi hodari anayetambulika ulimwenguni.

Kuelekea Wingilugha zaidi?

Maendeleo katika Umoja wa Mataifa

Mnamo 2020, Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kusimamia Wafanyakazi ilikamilisha Mfumo wa Lugha wa Umoja wa Mataifa, amabo unalenga kuimarisha mshikamano wa kujifunza na kutathmini stadi za lugha katika lugha zote sita rasmi[20]. Utekelezaji wake umeruhusu ujelezi upya wa mitaala ya kozi za lugha kwa viwango tofauti na miktadha tofauti ya matumizi. Hatimaye, inatarajiwa kwamba Mfumo huu utaimarisha utambuzi wa mahitaji ya lugha katika kuajiri watu.

Ofisi kuu ya Umoja wa Mataifa imetangaza juhudi nyingine za kusaidia wingilugha katika mwaka wa 2022 kama vile ukuzaji wa mfumo wa sera wa kimkakati na wenye mshikamano katika kuhakikisha wingilugha katika kazi ya Umoja wa Mataifa. IOF inasaidia ukuzaji wa Mfumo huu kupitia mchango unaolenga kuleta pamoja viwango vya juu vya utaalamu.

Mjadala unaoendelea katika Umoja wa Ulaya

Tangu kura ya Brexit, mamlaka ya Kiingereza katika taasisi yanabainika kuwa si ya haki. Sauti nyingi zimetolea[21] kupinga matumizi mapana ya lugha mabayo kwa sasa ni rasmi sawa na lugha za kitaifa, katika nchi mbili tu wanachana: Ireland na Malta Mjadala kuhusu wingilugha katika Umoja wa Ulaya pia umeanzishwa na janga la kiafya, ambalo lilisababisha Taasisi za Ulaya kutumia nyenzo za mawasiliano ya mtandaoni kupanga, katika majuma machache ya kwanza, mikutano ya mtandaoni kwa Kiingereza pekee katika ngazi zote, ikiwemo mikutano ya Baraza. Kufikia Mei 2020, Kamisheni ya Ulaya imeweka jukwaa ya kutangamana ambalo linaruhusu mtumizi ya lugha 32. Mwisho, Urais wa Ufaranza katika Umoja wa Ulaya katika nusu ya kwanza ya 2022, unapaswa kuwa nafasi ya kujadili mapendekezo mapya ya kurejesha usawa katika matumizi ya lugha rasmi.

[19]kifungu cha 23 cha Mkataba wa Olimpiki: Lugha rasmi za IOC ni Kifaransa na kiingerea. Katika vipindi vyote, ukalimani wa moja kwa moja utatolewa kwa Kifaransa, Kiingereza, Kijerumani, kihispania, kirusi na kiarabu.
Katika hali ambapo kuna tofauti baina ya matini ya Kifaransa na Kiingereza ya Mkataba wa Olimpiki na nyaraka nyingine yoyote ya IOC, matini ya Kifaransa itazingatiwa isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo katika maandishi.

[20]Voir QRcode.

[21]Mfano mmoja ni juhudi za kikundi cha Wahudumu wa Umma wa Ulaya ambao ni aazungumzaji wa Kifaransa, kwa jina "Carré bleu", ambao walituma barua wazi kwa Rais wa Kamisheni mnamo Septemba 2019 wakidai haki ya kufanya kazi kwa Kifaransa.

SEHEMU YA 2

SERA ZA LUGHA NA UFUNDISHAJI WA KIFARANSA DUNIANI

KIFARANSA, LUGHA YA ELIMU



KIFARANSA KAMA
LUGHA YA ELIMU

Kifaransa ni lugha ya ufundishaji katika mifumo ya elimu ya nchi 36 na serikali kote ulimwenguni (24 ambazo zinapatokana eneo la Afrika-Bahari Hindi na maeneo ya Mashariki ya Kati), ama peke yake au sambamba na lugha nyingine; asilimia 80% ya wanafunzi waliosajiliwa katika shule zinazotumia Kifaransa inapatikana barani AFrika, ambapo Kifaransa kwa jumla kinatumia kama lugha ya ufundishaji, lakini pia kama nyenzo ya mawasiliano baina ya jamii (ambapo lugha ya kwanza ni moja au zaidi, wakati mwingine baina ya mataifa, katika maeneo ambayo yana wingi wa lugha na tamaduni).

■ Chaguzi za sera ya lugha na hatua zinazoongozwa na Nchi.

Nchi na serikali za mataifa yanayozungumza Kifaransa Kusiki- hasa eneo kusini mwa Sagara na Bahari Hindi - zinahitaji sera za umma ambazo zinazingatia uhalisia wake wa kiisimujamii, na hivyo basi sharti zifanye uteuzi wa upangaji lugha ambao unaangazia masuala kadhaa: demokrasia ya kiisimu na heshima kwa haki za lugha za wachache; mshikamano wa kijamii na usambazaji baina ya vizazi tofauti; ufikiaji wa taarifa na haki kwa wote katika lugha zao za mama, n.k.

Bw. Jean-Marie Klinkenberg, profesa mstaafu katika Chuo kikuu cha Liège (Ubelgiji), anadokeza kwamba, “sera za lugha ni suala la ukuaji wa kibinafsi kama lilivyo la ukuaji wa pamoja” wakati lengo ni “kuoanisha soko la lugha na soko la ajira, kuongeza umilisi katika matumizi ya vifaa vya kujieleza (...); kuunganika na sera za ukufunzi, kwa zera za ulinzi na ukuaji wa mfanyakazi (kwa kuekebisha lugha ya mikataba, kazi, vifaa), hadi kwa sera ya ulinzi wa mteja (karatasi ya maagizo, usalama), hadi kwa sera ya mahusiano baina ya wananchi na mamlaka ya umma (usahilishaji wa lugha ya utawala na sheria, n.k.) sera ya nafasi sawa (kuzingatia jinsia katika majina ya kazi), sera ya utafiti na maendeleo, hasa katika uwanja wa dijitali, na sera juu ya ufikiaji wa mwananchi kwa taarifa ya kisasa na teknolojia ya mawasiliano.

Maamuzi mengi na matini zinazounga mkono tofauti za kiisimu tayari zinajumuisha vipengele vya sera ya lugha katika ngazi ya kitaifa katika nchi kadhaa barani Afrika (k.m. Afrika Kusini) au zinatambua haja ya kuunganisha mwelekeo wa ujozi- au wingilugha katika mifumo ya elimu ili kuimarisha ujifunzaji wa mapema (k.m. Mali, Burundi). Kwa kweli, kuna makubaliano ya hali ya juu kimataifa ya kulinda lugha zote na hatua zichukuliwe kukabiliana na changamoto ya “Ulinzi wa isimu-ikolojia”. Hata hivyo, ukweli unaonyesha kwamba sera chache za lugha zinatumika, na kwamba aghalabu zinashughulikia hadhi ya lugha (ambao athari zake mara nyingi si wazi, na mara nyingi hupimwa kidogo au kwa njia hafifu).

Isitoshe, wakati matini zinazalishwa na miradi inafadhiliwa na Nchi na washirika katika uwanja, karibu kila wakati zinajihusisha tu na kuingizwa kwa lugha fulani katika mfumo wa elimu na ujuzi wa kusoma na kuandika, hasa katika mzunguko msingi. Zaidi ya hayo, masuala ya sera za lugha kwa jumla hushughulikiwa na Nchi katika kiwango cha kitaifa, bila kuzingatia upekee wa kieneo, na kusambazwa chini ya usimamizi wa wizara ambao hutofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine.

Katika muktadha huu, jumuiya ya wazungumzaji wa Kifaransa husaidia mataifa wanachama na serikali kupitia kwa juhudi zinazojikita kwa lugha na sera za elimu, kuimarisha uwezo wa walimu, tathmini na ufunzaji wa manuzaa wa elimu ya ujozilugha (hasa kupitia mradi wake wa Shule na Lugha za kitaifa Afrika - ELAN).

■ Hali ya sasa kwa eneo na nchi

Takriban wanafunzi milioni 93 wanafunzishwa kwa Kifaransa ulimwenguni: takwimu ambazo zinaongezeka kidofo na zinathibitisha, kwanza, kwamba Kifaransa hakijapoteza hadhi yake kama lugha ya ufundishaji popote, na kwamba mifumo ya elimu ya nchi ambapo idadi ya watoto wanaohudhuria shule inaongezeka (kusini) inachukua idadi inayoongezeka (hata kama si wote wanasajiliwa).

Kimsingi, nchi ambapo Kifaransa ndio lugha rasmi pekee inayobeba uzito mkubwa ulimwenguni na miongoni mwake, idadi kubwa ya wanafunzi wa kifarana wanaishi katika bara Afrika, ikiwemo nchi ambapo Kifaransa si lugha rasmi (kama vile eneo la Kaskazini).

Mgawanyo wa wanafunzi wa lugha ya Kifaransa - 2022



Bara Bara la Ulaya linafuatia, kutokana na Ufaransa (Asilimia 91% ya wanafunzi wanafundishwa kwa Kifaransa), lakini pia katika Shirikisho la Wallonia-Brussels, Switzerland ambako Kifaransa kinazungumzwa, Luxembourg na Monaco.
Ikiwa Marekani ya Kaskazini inachukua nafasi ya tatu kutokana na Quebec na Canada kwa jumla, hatupaswi kusahau shima ya Haiti, hata kama kwenye takwimu zinazopatikana za hivi punde zaidi kuhusu nchi hii zimepitwa na wakati (2015-2016).
Mwisho, Lebanon inaongoza katika matumizi ya Kifaransa shuleni kwenye eneo la Afrika Kaskazini-Mashariki ya Kati, ingawa nafasi ya lugha hii kama mbinu ya ufundishaji haiwezi kupuuzwa - japo haijabainishwa wazi - katika nchi za kaskazini mwa Afrika.
Kuhusu sehemu ya Asia, idadi ndogo ya wanafunzi katika New Caledonia na Vanuatu inafanya iwe vigumu kubainisha ikilinganishwa na jumla ya watu.

KIFARANSA KAMA LUGHA
YA KIGENI

Mageuzi ya idadi ya wanafunzi wanaojifunza FLE yanatofautiana kulingana na eneo au nchi, kwa kiasi kikubwa kutokana na mapenzi ya mamlaka ya kitaifa kufanya ufundishaji wa lugha ya pili ya kigeni (au hata zaidi) kuwa wa lazima katika mifumo yao ya elimu. Nje ya nchi zinazozungumza Kiingereza, aghalabu huwa inabainishwa kwamba sera za umma hutoa nafasi tu kwa Kiingereza kama ugeni wa kiisimu na kitamaduni katika kukuza wananchi wachanga.

Mvuto wa lugha ya Kifaransa kwa vijana, wazazi wao na shuke pia ni kutokana na mitazamo kuhusu kile inaweza kutoa kwa masuala ya ajira, nafasi za kusoma ughaibuni, kufikia kazi zinazohusiana na utalii, mashirika ya kimataifa au mageuzi katika kampuni au utawala.
Hatua za kisiasa ni kigezo muhimu katika kuunda mifumo ya elimu na jamii zenye wingilugha ambazo zinaweza kukuza uwezekano wa vijana kuajiriwa, mafunzo na ukuaji wa kitaaluma katika masiha yao yote. Ia ni yule ambaye sharti akabiliane na mifumo mingi ya elimu, wakati mwingine kukiwa na shinikizo la wingi wa wanafunzi, na walimu wa Kifaransa ambao wanazidi kuwa nadra: walimu wanastaafu (ambapo wakati mwingine ni sababu tosha ya kuondoa Kifaransa katika shule), mtanziko wa wito wa kufundisha lugha (ikiwemo Kifaransa), ambazo aghalabu huwa za hiari kama lugha ya pili ya kigeni.

■ Kujifunza Kifaransa kama kigezo za sera za wingilugha katika elimu

Sera za elimu na za kiisimu huetekeleza wajibu mkubwa katika kujifunza lugha za kigeni, sio tu kwa shuruti ya mtaala wa shule, bali pia kwa mbinu ambazo zimetengwa kwazo. Tathmini mpya ya taaluma ya ualimu, ufufuaji na ukufunzi wa walimu vijana, ugatuzi nje ya miji mikubwa na uzingatiaji wa demokrasia katika ukufunzi wa wingilugha ni miongoni mwa changamoto ambazo huruhusu mifumo ya elimu kukabiliana na madai ya wananchi kwa kupendelea jamii za wingilugha.
Vivyo hivyo, chaguzi za sera ya kitaifa, kuambatana na mitazamo ya wingilugha inayopendelea lugha ta kitaifa na baina ya mataifa kwenye kiwango cha nchi, zina athari kwa kiwango cha uwazi wa mifumo ya elimu kwa masuala kama vile uhamaji wa kimataifa.

Katika muktadha huu, baadhi ya nchi hufanya marekebisho na kuanzisha Makubaliano ya ushirikiano baina ya washirika wengi au wawili wakipendelea ufufuaji na uhamishaji wa walimu, uimarishaji wa stadi zao za kiisimu na za kufundisha, utekelezaji wa miradi ya msaidizi wa lugha, uhamishaji wa wanafunzi n.k.

■ Ushirikiano baina ya washirika wawili na washirika wengi ili kusaidia ujifunzaji wa lugha ya Kifaransa

Makubaliano yaliyotiwa saini na Ufaransa aghalabu huwa thabiti katika kuimarisha ufunzaji wa Kifaransa. Kama sehemu ya sera za washirika wawili, Ufaransa huwezesha na kusaidia hatua za ushirikiano na mamlaka za mitaa kupitia ufadhili wa kitaifa au kieneo kama vile **FSPI**(Solidarity Fund for innovative projects, civil societies, La Francophonie and human development), kifaa ambacho hu-

wezesha ufadhili wa juhudi, hasa katika uwanja wa utamaduni, Kifaransa, elimu ya juu na utafiti.

Ushirkiano wa Ufaransa unajumuisha **LabelFrancÉducation** na mradi wa wasaidizi wa lugha nchini Ufaransa na ughaibuni. Ufarasa pia hutumia ujuzi wa timu zake za ufundishaji na wasimamizi - kwa mfano France Education International (FEI) - kuimarisha lugha ya Kifaransa katika shule za umma na za kibinafsi katika mfumo wa elimu wa kitaifa na katika shule za Kifaransa zilizoidhinishwa katika nchi husika.

Mnamo 2020, **Hazina ya Lugha ya Kifaransa** pia ilisaidia miradi 29 iliyoongozwa na Alliances françaises and Instituts français, including the Franco-Brazilian French Meetings on Tourism, a regional forum Génération LabelFrancÉducation in Bulgaria, and the "Les petits penseurs" project in the United States, aimed at school audiences.

Pamoja na maeneo yake 98 katika nchi 95, **Taasisi ya Kifaransa** huendesha jukwaa la IFprofs, ambalo huwaleta pamoja watalamu 42,000 kutoka nchi 105 (rasilimali wanazoshiriki 20,000) mnamo 2021. Rasilimali za jukwaa lake la Culturethèque (maktaba ya kidijitali) ziliwasaidia zaidi wa watumiaji 500,000 mnamo 2021 (yaani, idadi maradufu ikilinganishwa na 2019).

Inapaswa kutambuliwa kwamba mahudhurio ya kozi za FKE katika mtandao wa **Alliances françaises** 832 katika nchi 131, ukiwa na wanafunzi 490,000 wa FLE kote ulimwenguni mnamo 2019 (ikiwemo wanafunzi 111,000 katika kozi za FLE kwenye kampuni au taasisi) yamekua kwa alama 3.4% tangu 2018. Madagascar, India, Marekani, Mexico na Ufaransa ndizo nchi zinazoongoza ambapo Kifaransa kinasomwa kwenye Alliances françaises, zikifuatiwa na Uchina, Brazil, Colombia, Peru na Zimbabwe. Ingawa kozi za Kifaransa kwa umma kwa jumla hazikubadilika mnamo 2019, kozi zinazolenga biashara na taasisi ziliongezeka pakubwa mwakani (asilimia 16%).

Eneo la Marekani ya Kusini lipo katika nafasi ya kwanza likiwa na wanafunzi 130,000 waliosajiliwa katika mtandao wa Aliiances 172, na Bara la Ulaya, bara linaloongoza kwa uanzishaji wa Alliances françaises duniani likiwa na Alliances 236..

Kwa upande wake, IOF ina **vituo vitatu vya kieneo vya kufundisha Kifaransa (CREF)** : Vituo vya Ubora ambavyo hutoa nyenzo za hali ya juu katika uhandisi zinazotoa mafunzo na seminaa kwa kategoria zote za wataalamu wa lugha ya Kifaransa wanaofundisha katika mifumo ya elimu. Juhudi hii, ambayo ilijaribiwa kwanza mnamo 1993 katika Asia-Pacific (CREFAP), ilipanuliwa mnamo 2005 hadi Bara la Ulaya ya kati na ya mashariki (CREFECO) na, kuanzia 2021 hadi Afrika na Mashariki ya Kati (CREFA).
Programu hii inalenga zaidi ya walimu 50,000 na zaidi ya wanafunzi milioni 4 wa Kifaransa.

■ Cheti rasmi cha Stadi za Lugha ya Kifaransa

Miongoni mwa vifaa vya tathmini kwa walimu, mtihani wa APPRENDRE Ev@lang - unaofadhiliwa na FEI na AUF - ulizinduliwa mnamo 2021 katika toleo la ukufunzi, ili kutathmini kiwango cha stadi za lugha ya Kifaransa cha walimu katika mifumo ya elimu kwenye nchi 26 ambako Kifaransa kinazungumzwa.

Hata katika muktadha wa janga, utoaji wa cheti rasmi cha Lugha ya Kifaransa umezidi kupata idadi kubwa ya watahiniwa, hasa vijana, kukiwa na watahiniwa 214,121 (ikiwemo 108,376 katika muktadha wa mtihani wa DELF scolaire na kwa jinsi hiyo tathmini rasmi za lugha ndani ya mifumo ya elimu) mnamo 2021 katika ya jumla ya watahiniwa 381, 597 wa DELF-DALF. Idadi ya wanafunzi imekuwa ikiongezeka na itafikia upeo mnamo 2019 kukiwa na vijana watahiniwa 318,474 (ikiwemo 163,121 waliosajiliwa katika mtihani wa DELF scolaire) katika ya jumla ya watahiniwa 519,611 wa DELF-DALF, kuthibitisha ilhamu ya wanafunzi kupata cheti cha umilisi wao katika Kifaransa wakipata stashahada rasmi, hasa katika shule za upili.
Mtihani wa DELF scolaire hasa inavutia engi nchini Italia (asilimia 22% ya wasajiliwa wote mnamo 2019) na hasa nchini Ujerumani (asilimia 28% ya wasajiiwa).

■ Ukuzaji na matumizi ya nyenzo za kujifunza FOS/ Kifaransa cha Ufundi

Katika uwanja wa ushirikiano baina ya washiriki wawili kwa Kifaransa, nafasi inayochukuliwa na kozi za mafunzo yanayoishia katika stashahada kwa lengo la kitaaluma inahitaji kuangaziwa kwa njia ya kipekee. Kategoria ya wanafunzi wa Kifaransa “Kwa uamilifu maalum” (FOS) kwa hakika inaashiria mabadiliko ambayo yanashadidia umuhimu wa kujua Kifaransa, idai kubwa ya kozi hizi hutolewa katika elimu ya juu kupitia kwa programu za uzamili za “kutaalamisha”.

Katika nchi zote ulimwenguni, zinahusu nyanja zifuatazo: Lugha za kigeni tumizi, utamaduni na lugha ya mashirika ya Ulaya, ukalimani katika makongamano, tafsiri na istilahi maalum, mikakati ya mawasiliano baina ya tamaduni tofauti (kifasihi na kiisimu), lugha za kisasa na mawasiliano ya kimataifa, kufundisha Kifaransa, teknolojia za lugha na tafsiri za mitambo n.k.
Lugha ya Kifaransa pia aghalabu hupatikana kuwa sehemu muhimu ya ukufunzi unaohusu utawala wa umma, mahusiano ya kimataifa, diplomasia, au ulinzi na masuala ya usalama (hasa barani Afrika).

Kule barai Ulaya, Afrika Kaskazini, na kwa kiwango kidogo, Asia, taaluma zinazohusika zinavuka sekta ambazo inahusiana moja kwa moja na lugha: usanifu wa majengo, ukulima na biashara kilimo, uanahabari, udaktari na afya, usimamizi, uhandisi wa mifumo ya viwanda, utalii, mauzo, fedha na udhibiti, sheria ya kimataiga (ya umma na binafsi), uchumi na usimamizi, hisabati na sayansi ya kompyuta, uhandisi wa kemikali, utaratibu wa kimataifa na usafiri, sayansi ya kisiasa, nk.

Programu nyingine na vifaa kama vile Professional **French Diplomas** (DFP) zimesanifiwa na kukuzwa na kituo cha Biashara cha Ufaransa cha Baraza la Biashara na Viwanda la Paris, kuanzia hapa litatajwa kama "FDA-CCIP" - zinajikita kwa ukufunzi wa wakufunzi, kukuza programu za ukufunzi na utahini katika FOS/Kifaransa cha kitaaluma - huwezesha kuimarisha umilisi wa Kifaransa hasa katika biashara, mahusiano ya kimataifa, na sekta za utalii/hoteli/biashara/mikahawa kupitia kwa mafunzo kwa Kifaransa ambayo yametolea kimataifa.

Kwa mujibu wa **FDA-CCIP**,maombi ya mafunzo katika Kifaransa cha ufundi hayajadidimia licha ya changamoto ya kiafya ambayo imeathiri vituo vya lugha kwa vile kuanzishwa kwa masomo ya mbali pia kumewezesha kutoa mafunzo yaliyoandaliwa kukimu mahitaji mapya.
Miongoni mwa dalili za kukua kwa ilhamu katika professional French diplomas (DFP), tunatambua mageuzi ya maombi ya kuidhinishwa kwa vituo vya lugha kuandaa vipindi vya professional French diploma (yameongezeka kutoka 30 mnamo 2018 hadi 70 mnamo 2020) na ilhamu katika kuandaa mafunzo ya wakufunzi na kuandaa utahini katika Kifaransa cha ufundi.

Kati ya zaidi ya wanafunzi 23,000 ambao walifanya mojawapo ya DFPs baina ya 2016 na nusu ya kwanza ya 2021, asilimia 72% walikuwa wanasomea DFP ya biashara; asilimia 13% walikuwa wanasomea DFP ya uhazili; asilimia 6% wakisomea DFP ya Utalii, biashara ya Hoteli na Mikahawa; na asilimia 5.5% wakisomea DFP katika Mahusiano ya kimataifa. Asilimia themanini ya watahiniwa walitoka Switzerland, Ufaransa, Italia, Marekani, Misri, Algeria, Spain, Lebanon, Austria, Urusi na Ubelgiji.

Ruwaza kuu zilizotambuliwa zinaonyesha kwamba bara Bara la Ulaya bado liko mbele katika maombi ya mafunzo na utahini katika Kifaransa cha Ufundi. Ilhamu inadhihirika pia nchini Kenya, India na Mexico. Maombi yangali thabiti katika Marekani ya Kaskazini, na yako chini sana katika bara Asia ambapo uhusiano baina ya umilisi wa Kifaransa na Umilisi wa kitaaluma unaonekana unahitaji ukarabati.

Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa kufunza FOS ambazo pia zimekuzwa, tunaweza kutambua uzinduzi wa **Clés du français pro** mnamo Machi 2021 na FDA-CCIP na Taasisi ya Kifaransa, kusaidia mtandao wa vituo vya lugha ya Kifaransa kwa kuandamana na ukuzaji wa ofa ya kozi katika Ufundi wa Kifaransa.

Ofa ya **TV5MONDE** pia imeimarishwa na nyenzo za kielimu zinazoangazia sekta mbalimbali za kitaaluma (biashara, utalii, hoteli na mikahawa, mitindo na usanifu, mahusiano ya kimataifa na diplomasia), na makala za kielimu kwa kozi za Kifaransa cha ufundi (biashara ya hoteli, mauzo, utalii) zilizozalisja na TV5 Québec Canada kwa ufadhili wa Office québécois de la langue française. Mradi ambao unaendelea, kwa ushirikiano na Cité internationale de la langue française in Villers-Cotterêts (Ufaransa).

Nguvu ya FOS au mafunzo ya Kifaransa cha ufundi ughaibuni, au angalau uwezo wake, hivyo basi hauna shaka, hasa kutokana na mabadiliko ya mifumo ya mafunzo na utahini iliyoshuhudiwa na FDA-CCIP, fursa ya mseto wa umma ambao unawakilishwa kwa vituo vya lugha na mafunzo, na zaidi ya yote kuibuka kwa umma mpya “ulio na msukumo halisi wa kutaka kufanya kazi kwa Kifaransa” - tukimnukuu Bi. Florence Mourlhon-Dallies, ambaye pia anaeleza: “Tuko na (...) wanafunzi wachache wa viwango vya juu, lakini maombi mengi zaidi ya utahini wa kati na ufundi. "

■ Hadhi na mienendo kwa maeneo na nchi

Mnamo 2018, idadi ya wanafunzi wa Kifaransa ulimwenguni ilikuwa juu ya watu **milioni 51** kwa wanafunzi katika shule za umma na za kibinafsi, vyuo anuwai, shule za upili na taasisi za eimu ya juu, pamoja na usajili katika taasisi za lugha ya kigeni au vituo nje ya mfumo wa shule. Uongozi wa eneo la Afrika Kaskazini - Mashariki ya Kati unazidi ukiwa na asilimia 44% ya wanafunzi wa FLE katika mifumo ya elimu, likifuatwa na eneo la Kusini mwa Sahara-Bahari Hindi (20%), Bara la Ulaya (19%), Marekani na Karibia (9%) na Asia-Oceania (3%).

Kwa jumla, idadi ya wanafunzi wa FLE imepungua kidogo sana kwa asilimia 0.1% tangu 2018, hasa ikiashiria kupungua kwa kasi kwa ujifunzaji wa Kifaransa ulioshuhudiwa Bara la Ulaya (-10%). Kwa upande mwingine, maeneo mengine ulimwenguni yanashuhudia ongezeko la wastani katika idadi ya wanafunzi wa Kifaransa.

Uzito wa Kaskazini mwa Afrika pekee ni mkubwa, kwa vila Algeria, Morocco na Tunisia peke yake huwakilisha zaidi ya wanafunzi milioni 17 wa FLE. Idadi kubwa ya wanafunzi waliohesabiwa kwa kweli wanafunzwa kwa njia amnayo pakubwa inafanana na ile iliyoelezwa katika mifumo mingine ya elimu kuwa "ujozilugha", au hata "kwa Kifaransa" kwa baadhi ya masomo na kwa viwango fulani vya masomo, hata hivyo, kielezo "lugha ya kigeni" kinachotumikwa kwa Kifaransa katika nchi hizi kinaheshimiwa.

Afrika ambayo haizungumzi Kifaransa ingali inawakilisha asilimai 25% ya jumla ya usajili, huku nchi zikitumia uzungumzaji wa Kifaransa kwa kiasi fulani (bila kujali iwapo wao ni wanachama wa IOF) katika mtazamo wa ushirikiano baina ya maeneo. Cameroon (kwa sehemu yake inayozungumza Kiingereza) Mozambique na Ghana ni miongoni mwake pamoja na Uganda, Angola, Afrika Kusini na Kenya. Katika eneo la Kusini mwa Sahar, ukuaji katika kipindi kilichotafitiwa unaonekana kuwa ulisukumwa na Angola, Ethiopia (kabla ya mgogoro), Sao Tome na Principe na Ushelisheli.

Bara la Ulaya ingali bado ni ngome ya ujifunzaji wa lugha ya Kifaransa ambapo Italia na Romania zipo katika nafasi ya kwanza (kwa kiasi) pamoja na Ujerumani, Uhispania, na sehemu za Ubelgiji ambapo Kifaransa hakizungumzwi na Switzerland, Uholanzi, Ugiriki na Ureno. Nchi zinazozungumza Kiingereza (Uingereza na Ireland) huku Kifaransa kikitumika kama lugha ya kwanza ya kigeni pia zilijumuisha zaidi ya wanafunzi milioni 0,5 wa FLE**.**

Mabadiliko katika usajili wa kifransa kama Lugha ya kigeni (FLE) kati ya 2018 na 2022 (upeo wa mara kwa mara)



Nje ya nchi zinazozungumza Kiingereza, wakati lugha moja pekee ya kigeni ni ya lazima, Kiingereza hushinda (wakati haijawekwa bayana kuwa lazima na mamlaka za elimu, ambayo ndiyo hali ya kawaida zaidi), na uwezekano wa kutelekeza lugha ya kigeni mapema katika shule, kama ilivyo Uingereza, umechangia kupungua kwa idadi ya wanafunzi wa FLE.

Katika mazingira ya kiisimu yenye ushindani mkubwa ya nchi za Ulaya, uhusiano wa kitamaduni, ukaribu wa kijiografia, ugumu mkubwa au mdogo unaohusishwa na lugha tofauti zilizopo "sokoni" na sifa zinazotolewa kwao - kama vile sera za kujitolea zaidi za mamlaka ya elimu - kuelekeza uchaguzi wa wanafunzi na wazazi wao. Wakati lugha ya pili (au ya tatu) ya kigeni si ya lazima, ushindani unazidishwa baina ya Kifaransa, kihispania, kirusi, Kijerumani na kiitaliano...na Kifaransa wakati mwingine hakishindi.

Bara la Amerika na visiwa vya Karibia huchukua nafasi ya tatu katika FLE huku Canada (bila kujumuisha Quebec) na Marekani, ikifuatiwa na Costa Rica, Brazil, Mexico na Argentina, miongoni mwa nchi nyingine. Idadi ya jumla ya wanafuni imeongezeka kwa asilimia 31.7% katika eneo hili, kutokana na manufaa ya ongezeko kubwa katika ujifunzaji wa Kifaransa nchini Costa Rica na Chile.

Eneo la Asia-Oceania limekuwa na idadi ndogo ya wanafunzi wa FLE, japo baadhi ya nchi katika eneo hili, kama vile Australia, India, Uchina, Laos, Cambodia, Azerbaijan na Vietinamu, zina idadi kubwa ya wanafunzi (takribana 50,000) japo idadi hii ni ya chini ikilinganishwa na jumla ya wanafunzi. Cambodia, Uchina, Laos, Malaysia, Thailand, na Vanuatu zimeongeza ukuaji wa jumla na kufidia baadhi ya kupungua nchini Japani na Kazakhstan, kwa mfano.

SEHEMU YA 3

LUGHA YA KIFARANSA, UTAMADUNI NA ULIMWENGU WA DIJITALI

NAFASI YA KIFARANSA MTANDAONI

Muhtasari wa maendeleo

Muundo uliotumika katika toleo lililopita umeboreshwa katika baadhi ya vipengele (chanzo bora cha data ya kiisimu kidemografia, kughairiwa kwa mojawapo ya mapendeleo makuu ya utafiti kutokana na upatikanaji wa data ya wazungumzaji wa lugha ya pili kulingana na nchi, uzingatiaji bora wa wingilugha wa watu binafsi[22] na kuendelea kwa uchanganuzi wa utaratibu wa upendeleo, usioepukika katika aina hii ya kazi, na utafutaji wa njia za kukabiliana nao) na mkusanyiko wa data umesasishwa mnamo Mei 2021.

Ingawa Kifaransa bado ni lugha ya nne[23] mtandaoni.

- Sasa kinaambatana, na pengine kushindwa, na Kihindi, ambacho kinakua kwa kasi; na
- Uongozi wake juu ya lugha zifuatazo (kwa sasa: kireno, kirusi, kiarabu, Kijerumani, kijapani na Malay) umepunguzwa pakubwa, kutokana na muungano wa masuala haya mawili **:**

1. Viwango vya uunganifu wa intaneti kwa wazungumzaji wa Kifaransa katika nchi zilizoendelea karibu vinafikia kiwango kifu (wastani wa 85%), na kuwacha nafasi ndogo ya kukua; na
2. Mgawanyo wa kidijitali katika nchi za Afrika zinazozungumza lugha ya Kifaransa ni wa polepole sana kuliko wastani wa ukuaji wa muunganisho duniani kote.

IInaelekea kwamba kupungua huku katika Kifaransa, ambako kulikuwa kumeshuhudiwa katika tathmini zilizofanywa mnamo 2019 na 2020 ni matokeo ya tofauti kubwa baina ya kiwango cha wastani cha ukuaji wa uunganifu kwa kila nchi na kile cha nchi kadhaa barani Afrika ambako Kifaransa kinazungumzwa. Pengo hili pia ni pana mno katika nchi za Asia, kwa kiwango kikubwa, nchi za Uarabuni, ambazo zinaonyesha viwango vya uunganifu vinavyoelekea vile vya mataifa ya Magharibi.

Kwa muda mrefu, utabiri wa ukuaji wa kidemografia barani Afrika utasaidia uwepo wa Kifaransa mtandaoni kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Hata hivyo, iwapo Mgawanyo wa kidijitali utaendelea kuwa mpana katika sehemu za Afrika zinazozungumza Kifaransa, uwepo wa Kifaransa mtandaoni utaathirika kwa kipindi kifupi.

[22]Mnamo 2018, kiwango cha 25% cha muundo wa wingilugha kichukuliwa, na matokeo ya lugha ya kwanza na ya pili (L1+L2) kwa hivyo yalitokana na asilimia 125% ili kuwajibikia wingilugha. Katika toleo hili mpya la 2022, kutokana na data ya Ethnologue, kipengele cha wingilugha kinaongezeka hadi asilimia 43%.

[23]Kati ya lugha 329 lzilizo na zaidi ya Wazungumzaji milioni 1

UFAFANUZI WA VIASHIRIA VIKUU UNAOTOLEWA NA MFUMO UNGALI SAWA NA, HASA, TUNABAKI NA KIASHIRIA CHA "NGUVU" AMBACHO KINAENDANA NA WASTANI WA VIASHIRIA SITA :

WATUMIAJI WA INTANETI
=
Asilimia za kilimwengu asilimia za kilimwengu za Wazungumzaji waliounganishwa na tovuti za lugha katika (Inapatikana kwa kupima Wavuti (inapatikana kutokana na majukwaa na programu

WINGI
=
Data ya uunganifu kutoka kwa programu hizi (k.m. asilimia
Kwa nchi na kuripoti data msambao wa wateja kwa

MATUMIZI
=
sifa anuwa za kidemografia na kiisimu (za watumiaji kwa kila nchi) mitandao ya kijamii

ISHARA
=
mabadiliko ya kipimo cha asilimia ya ulimwengu ua uwepo wake
orodha ya nchi katika gombowavuti kama lugha ya mapatano

YALIYOMO
=
katika asilimia kwa kila lugha

MAPATANO
=
wingi wa viashiria tofauti kwa programu au wa jumuiya ya taarifa kama lugha ya
(k.m. Ubora wa tafsiri ya mtandaoni.
e-government)

Kiashiria hiki huunganisha vigezo vyote ambavyo huashirikia uwepo wa lugha mtandaoni.

Mseto wa vigezo (uliorekebishwa kuondoa upendeleo katika vyanzo) ulipatikana kwenye muundo wa mazao unatoa orodha ifuatayo ya jumla:

RANG	LANGUE	PRÉSENCE
1	Kiingereza	25,00 %
2	*kichina*	15,00 %
3	kihispania	7,00 %
4	Kifaransa	3,50 %
4	Kihindi	3,50 %
6	kireno	3,00 %
6	kirusi	3,00 %
8	*kiarabu*	2,50 %
8	Kijerumani	2,50 %
8	kijapani	2,50 %
11	*kimalay*	1,80 %
12	kiitaliano	1,40 %
13	kituruki	1,20 %
14	kikora	1,20 %
15	kibengali	1,20 %
	ZINGINE	**25,70 %**

Manufaa ya lugha ya Kifaransa katika ulimwengu wa dijitali

Viashiri viwili muhimu zaidi vya lugha ya Kifaransa katika muktadha huu ni :

1. Uwiano wa (L1+L2)/L1, alama ya marudio ya matumizi ya lugha kama lugha ya pili, ambayo Kifaransa ni lugha ya tano duniani; na
2. Idadi ya nchi ambapo kuna Wazungumzaji wa lugha fulani, ambayo Kifaransa ni ya pili kwa Kiingereza[24].

Hii inafanya iwezekane kujaza kiashiria kipya: **kiwango cha utandawazi wa lugha (DML).** Inajelezwa ifuatavyo: DML = (L1+L2)/L1 x asilimia ya nchi ambapo lugha husika inazungumzwa.

kiashiriki hiki kipya kinatuwezesha kupanga nchi kwa kuunganisha vigezo hivi viwili ambavyo vinatambua eneo la kijiografia na kidemografia la lugha: muungano huu huzalisha idadi ambayo tafsiri yake katika asilimia huonyesha daraja na kusisitiza tofauti. DML kwa kuundwa, inajisimamia kutokana na uwepo wa lugha mtandaoni.

Lugha ambazo uwiano (L1+L2)/L1 ni zaidi ya 2.5 ni, kwa utaratibu, Dioula, Swahili, Kiingereza, Bamanakan, Kifaransa, Urdu, Malay, kisotho cha Kaskazini na Thai. Na lugha zinazozungumzwa katika aidi ya nchi 35 ni Kiingereza, Kifaransa, kihispania na kiarabu.

Kuzidisha idadi ya daraja la lugha ya utandawazi (DML) kwa asilimia ya wazungumzaji waliounganishwa hutoa **kiwango cha lugha cha utandawazi wa mtandao** (DCL) (DCL = DML x %Conn.), kiashirio ambacho huunganisha nguvu za utandawazi wa lugha katika ulimwengu wa kidijitali. Kwa kuongeza mweleko wa wastani wa muunganisho kwenye Mtandao, DCL husahihisha idadi ya DML kwa kuzingatia uwepo katika Mtandao wa kila lugha.

Dira ya mgawanyo wa asilimia inatuwezesha kupima tofauti na kuona kwamba lugha ya Kiingereza na Kifaransa zina uongozi wa wazi juu ya lugha zingine, kulingana na kigezo hiki kinachoonyesha jinsi lugha inavyoingizwa katika harakati za sasa za utandawazi (DML) na katika maendeleo kuelekea kwa wingilugha ambao unabebwa na Mtandao (DCL). Idadi zilizoonyeshwa kwa asilimia zinaonyesha msambao wa viashiria viwili kati ya lugha zote zinazozingatiwa: kwa hivyo, Kiingereza na Kifaransa kwa pamoja zinashughulikia karibu asilimia 25% ya usambazaji huu, na ukingo mkubwa wa umbali mbele ya Kijerumani, kirusi na kihispania, ikifuatiwa na kiarabu, Malay, kiitaliano na kichina.

[24]Imehesabiwa kwa lugha 329 zilizo na zaidi ya wazungumzaji milioni 1 wa L1, na data ya muunganisho wa Septemba 2021, kulingana na nchi 215 (au maeneo) iliyochaguliwa katika muundo.

LUGHA	DML	DML%	DCL	DCL%
Kiingereza	2,51	12,68 %	1,61	14,24 %
Kifaransa	1,69	8,52 %	1,09	9,66 %
Kijerumani	0,48	2,45 %	0,42	3,75 %
kirusi	0,40	2,01 %	0,31	2,76 %
kihispania	0,37	1,90 %	0,27	2,40 %
kiarabu	0,30	1,51 %	0,18	1,56 %
kimalay	0,33	1,69 %	0,17	1,51 %
kiitaliano	0,22	1,13 %	0,17	1,50 %
kichina	0,25	1,27 %	0,16	1,46 %

Nafasi ya lugha nyingine

Zifuatazo ni lugha mbazo zimeunganishwa zaidi mtandaoni (data isiyo na upendeleo), ikilinganishwa na asilimia ya Kifaransa ambayo ni 65.5% :

Lugha	Asili mia ya wazungumzaji nchini mwao
kinorwiji	97,87 %
kidanishi	97,83 %
kiswedishi	93,49 %
kijapani	92,62 %
kiholanzi	92,02 %
kiluxemburgo	91,90 %
Kijerumani ya Uswisi	91,56 %
kicatalani	90,50 %
kifemish ya magharibi	90,43 %

Hali ya Kiingereza

Kwa upande wa Kiingereza, nafasi yake inaendelea kupungua kutoka asilimia 30% mwaka wa 2017 hadi 25% mwaka wa 2021, hata kama vyombo vya habari, vinavyotegemea matokeo yenye upendeleo mkubwa, kwa kukosa kuzingatia wingilugha kwa uzito, vitaendelea kutangaza takwimu zaidi ya asilimia 50%. Kwa kweli, mtandao umebadilika pakubwa katika miaka kumi iliyopita kukiwa na ongezeko kubwa la lugha za Asia na kiarabu! Kuhusu asilimia ya kimataifa ya wazungumzaji wa Kiingereza waliounganishwa (L1+L2), ilikadiriwa na Observatory of Linguistic and Cultural Diversity on the Internet mnamo 2007 kuwa asilimia 32%, na sasa imeshuka hadi asilimia 15%.

MAUDHUI YA UTAMADUNI WA KIFARANSA MTANDAONI : THAMANI NA CHANGAMOTO ZA KUGUNDULIWA

Licha ya tofauti yake kubwa, maudhui ya kitamaduni na kisanii na maonyesho ya nafasi ya wazungumzaji wa Kifaransa yapo kidogo na yanaweza kupatikana mtandaoni[25]. Uwekaji wa uenezaji na usambazaji wa utamaduni katika majukwaa umetatiza mifumo ya jadi katika uhusiano kati ya ugavi na mahitaji, hasa kwa manufaa ya GAFAM[26]. Mduara huu mdogo wa washirika wa kimataifa unatumia fursa ya maendeleo ya kiteknolojia kudhibiti na kukusanya usambazaji wa kitamaduni, na kutishia ugunduzi wa uhakika wa maudhui ya kitamaduni ya lugha ya Kifaransa.

■ Mienendo mikuu katika nyanja za utamaduni na usanii[27]

Leo CCI hutao mchango muhimu kwa ajira katika uchumi wa ulimwengu. Mabadiliko yake ya kidijitali yanaathiri nchi zote na yanaenda sambamba na mabadiliko ya kiteknolojia na mageuzi ya matumizi ya idadi ya watu ambayo yanazidi kuwa na vifaa na kushikamana. Licha ya tofauti kubwa kati ya maeneo, sehemu kubwa ya watu duniani sasa wanafikia CCI kupitia njia za kidijitali.

Sekta ya sinema, muziki na maonoskizi imekuwa ikigeukia teknolojia ya dijitali kwa miaka kadhaa. Washirika wakuu wa kimataifa wameshajipanga. Wanatawala soko na kushikilia sehemu kubwa ya watazamaji.

Kwenye upande wa jumuiya ya wazungumzaji wa Kifaransa, juhudi zinazopendelea tofauti zimejitokeza (TV5MONDEPlus ilizinduliwa mnamo Septemba 2020, La Francophonie TV5MONDEplus Fund, ilizinduliwa mnamo Machi 2021),

[25]State of the art of discoverability and access to francophone cultural content on the Internet, 2020. Voir QRcode.

[26]Ufupisho unaotumika unaoundwa kutokana na herufi za kwanza za makundi makubwa: Google, Amazon, Facebook, Apple, Microsoft, n.k, na tunaweza kuongezea Spotify, Deezer, n.k.

[27]Cultural and creative industries in the world in the digital age, Study carried out for the IOF by Post-Advisors, June 2021. Voir QRcode.

UGUNDUZI NI NINI?

Hili wazo jipya Kutoka Quebec/Canada, lililobuniwa na kuboreshwa tangu mwaka wa 2016

Unafanua mchakato wa mkutano kati ya madhui na hadhira katika mazingira ya kidigitali

Inajumuisha :

- ■ Asili ya maudhui iliyo au inayopatikana mtandaoni kwa urahisi na yeyote ambaye anatafuta akitumia injini ya mitandao ;
- ■ Uwezekano mkubwa wa kugundua maudhui ambayo hayakutarajiwa au kutambulika kuwa yalikuwemo ;
- ■ Mapendekezo ya maudhui ya kitamaduni bila kuwepo kwa ombi lolote kutoka kwa mtumizi.

Kwa hivyo ugunduzi unajumuisha maudhui ya kitamaduni, mahitaji :

- ■ ugunduzi (marejeleo na kuorodhesha)
- ■ upatikanaji (kuendeleza na kutoa ofa za kutosha)
- ■ mapendekezo (uboreshaji na ukuzaji wa mwonekano).

■ Michakato ya kiufundi ya ugunduzi wa kimfumo

Majilio ya Wavuti 3.0 yaliwezesha kuibuka kwa data iliyopangwa, kusanifiwa na inayoweza kusomeka na kompyuta. Leo, mashine huunganisha, kuunda, kutumia na kushiriki taarifa ambayo inaonekana zaidi na inaweza kutumika vyema zaidi. Mbinu mbili hukuza ugunduzi wa maudhui mtandaoni: Data, kitovu cha vita na ambayo kila aina ina vipimo vyake; Kanuni, kwenye kiini cha mfumo wa mapendekezo.

Metadata bora na inayoweza kushirikiana (inayoweza kupitishwa na kubadilishana kati ya mifumo tofauti) ni suala la msingi kwa ugunduzi wa mtandaoni wa maudhui ya kitamaduni.

Idadi ya watu duniani wanaoweza kuingia Mtandaoni



Asili mia **53.6** ya walimwengu waliweza kuingia mtandaoni katika mwaka wa 2017.

Asili mia **47%** katika nchi zinazoendelea.

Asili mia **19.1** katika nchi zilizo kiwango cha chini cha maendeleo ya chini

Chanzo : *Utafiti wa Post Advisors ,The World's Cultural and Creative Industries in the digital age*, Juni 2021

CCIs, sekta ya muhimu katika uchumi wa dunia

Dola bilioni 2,250
ya michango ya kila mwaka kwa viwanda vya wabunifu kuelekea uchumi wa dunia (GDP), yaani asili mia **2.6%**.

Nafasi za kazi milioni 30
Duniani kote, ikiwemo sekta isiyo rasmi.

Asili mia 20 ya vijana
Asili mia 20 ya wafanya kazi katika sekta ya CCI waliyo na kati ya miaka 15 na 29 .

Asili mia 45% ni wanawake
Asili mia 45% ya wafanya kazi wa CCI ni wanawake.

Chanzo : *Utafiti wa Post Advisors The World's Cultural and Creative Industries in the Digital Age*, Juni 2021

Video na takwimu za kupata muziki



Asili mia **62%** ya kutazama filamu duniani katika mtandao was **Netflix** (kulingana na IOF, 2020)

Weteja milioni **345** wa Spotify kila mwezi katika mwaka wa 2021 *(kulingana na Les Échos)*

Video za masaa **500** yaliwekwa mtandaoni kila dakika *(kulingana na Statistica)*

Kuonyesha video inawakilisha asili mia **61** ya shughuli za mtandaoni. *(kulingana na Statistica)*

Chanzo : *Utafiti wa Post Advisors The World's Cultural and Creative Industries in the Digital Age*, Juni 2021

Changamoto dhidi ya ugunduzi kupitia takwimu kadhaa



KURUDIWA
asili mia 40 ya **mauzo ya vitabu** katika mtandao wa Amazon yanatokana na ingini yake ya kutafuta maelezo (IOF, 2020)



UPATIKANAJIT
asili mia 26 ya maudhui yaliyo katika huduma ya **video-on-demand** katika Umoja wa Ulaya katika mwaka wa 2018 ilitoka barani Ulaya. (IOF 2020).



MAPENDEKEZO
asili mia 60 of ya **Maudhui yaliyo kwenye Netflix** inatokana na mapendekezo yaliyo katika mtandao wao. (IOF, 2020)

Chanzo : *Utafiti wa Post Advisors The World's Cultural and Creative Industries in the Digital Age*, Juni 2021

■ Ugunduzi, suala la hali ya uhuru na usimamizi wa watendaji wengi

Hatari za usanifishaji wa matumizi ya utamaduni na upoteaji wa manufaa ya kiuchumi ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya kila jamii sasa yana maana.

Ugunduzi unahusisha masuala kadhaa yanayohusiana na uhuru wa Nchi: uhifadhi wa utambulisho wa kitamaduni; ukuzaji na ufikiaji wa masoko ya kimataifa kwa mazao ya kidijitali kitamaduni ya kieneo na kitaifa; uwezo wa mamlka ya Nchi kuingilia kupitia kwa utekelezaji wa mikakati toshelevu ya kisiasa (udhibiti). Mkakati wa Digital Francophonie 2022-2026 umetoholewa kutoka La Francophonie mnamo Desemba 2021[28] unazingatia changamoto za aina mbalimbali unazozalisha.

Mataifa wanachama na srikali za Jumuiya ya wazungumzaji wa Kifaransa, wnaviwanda na washirika wa kibinafsi, mashirika yasiyokuwa ya serikali, na mashirika ya kimataifa kwa pamoja yanajihusisha na suala la ugunduzi.

Kutoka : *Juhudi kwa ajili ya wazungumzaji wa Kifaransa kwa ugunduzi wa Maudhui ya Kifaransa mtandaoni*, IOF



[28]Voir QRcode

VITABU NA WAANDISHI KATIKA LUGHA YA KIFARANSA

Fasihi, bila shaka, ni mojawapo wa mahali pazuri zaidi kwa tofauti za kitamaduni za Kifaransa kunawiri. Kwenye kitovu cha masuala ya ubunifu na nguvu ya lugha ya Kifaransa, kitabu, katika hali zake zote, ikiwemo dijitali, ni zao la kile tunachokiita sekta ya utamaduni. Chini ya masuala haya mawili, utamaduni na uchumi, maoni yametolewa kwa muda mrefu na yanadhihirisha mandhari yaliyochochewa na ukinzani, wakati mwingine mivutano, ingawa ni tajiri sana na yamejaa matumaini.

■ Mkutano mkuu wa Vitabu vyaKifaransa Duniani

Mkutano mkuu wa Vitabu vya Kifaransa Duniani ulifanyika mnamo 23–24 Septemba 2021 mjinie Tunis. Uliletwaleta pamoja (moja kwa moja na kwa mtandao) zaidi ya washiriki mia nne - waandishi, waigizaji katika msururu wa vitabu, viongozi wa kisiasa na wa mashirika - kutoka pembe zote za ulimwengu wa Kifaransa. Iliyoandaliwa na Ufaransa kwa ushirikiano na mataifa sita au serikali (Côte d'Ivoire, Jamhuri ya Guinea, Quebec, Shirikisho la Uswizi, Tunisia, Shirikisho la Wallonia-Brussels), pamoja na Shirika la kimataifa la Jumuiya ya wazungumzaji wa Kifaransa, walihusisha karibu wadau 1,000 wa vitabu katika nchi 45 tofauti na kusababisha kutambuliwa kwa mapendekezo kumi ya kipaumbele ya kutekelezwa (kati ya 50 iliyoainishwa hapo awali[29]).

Wakirejelea mapendekezo haya, na tayari kuchukua baadhi yao, mawaziri tisa[30] wanaosimamia utamaduni na vitabu, wanaowakilisha taifa au serikali yao, walipitisha azimio la pamoja mwishoni mwa kazi, ambalo lilitaja haswa kukuza upatikanaji wa vitabu na kusoma, msaada kwa utunzi kwa kuhakikisha malipo ya haki kwa waandishi, tafsiri katika lugha ya Kifaransa, kuboresha usambazaji wa kazi na waandishi, na kuimarisha dhamira za maktaba.

Kama utangulizi wa Mkutano Mkuu, tafiti kadhaa zilifanywa ili kuelewa vyema sifa za soko la uchapishaji la lugha ya Kifaransa na kutarajia maendeleo ya siku zijazo: muhtasari saba wa kikanda[31] wa soko la uchapishaji la lugha ya Kifaransa uliofanywa na Bureau international de l'édition française (BIEF) na utafiti unaotarajiwa kufanywa na kampuni ya BearingPoint, wenye anwani "kitabu cha lugha ya Kifaransa mnamo 2030 na 2050[32]".

Matokeo ya tafiti hizi yametoa sababu kwa washiriki wa Mkutano Mkuu ambao walisisitiza juu ya mambo kadhaa: kupata mfumo wa kisheria, kuwezesha usambazaji wa malighafi na vitabu vyenyewe, haja ya kuboresha ujuzi wa pamoja na fursa za mawasiliano kati ya wataalamu. Katika hoja hii ya mwisho, uanzishwaji wa mtandao wa kidijitali wa washirika wa kitabu katika lugha ya Kifaransa [33] na IOF unachangia maendeleo.

Fursa ya kukumbuka pia mipango iliyotengenezwa na IOF ambayo inaingilia kati katika viwango kadhaa vya "mnyororo wa vitabu": uundaji, uzalishaji, usambazaji na ukuzaji. Pia inaangazia uungaji mkono wake wa sera za usomaji wa umma nchini kupitia mitandao ya vituo vya kusoma na shughuli za kitamaduni (CLACs) vilivyopo katika baadhi ya nchi ishirini za Kusini, pamoja na Prix des cinq continents de la Francophonie, ambayo kila mwaka hutuza mwandishi anayezungumza Kifaransa na kumruhusu kung'aa kimataifa kupitia "ziara za kifasihi" kote ulimwenguni.

■ Kongamano la Waandishi wa Lugha ya Kifaransa

Ilianzishwa mwaka wa 2019 na Leïla Slimani na marehemu Michel Le Bris, Kongamano hili la Dunia la waandishi wanaozungumza Kifaransa pia lilifanyika Tunis mnamo 25 - 26 Septemba 2021 kwa msaada, miongoni mwa wengine, wa IOF. Kwa mwaliko wa Kamati ya Fasihi iliyojumuisha Leila Slimani, Fawzia Zouari, Laurent Gaudé, Yanick Lahens, Felwine Sarr na - hadi Januari 2021 - Michel Le Bris, waandishi wapatao thelathini kutoka mabara matano walishiriki, moja kwa moja au kupitia mtandaoni, katika mpangilio wa mikahawa ya fasihi, mikutano, mahojiano makuu na mijadala ya pamoja.

[29]Kwa ajili ya mabadiliko katika kitabu cha lugha ya Kifaransa ulimwenguni: Book of proposals and 10 priority recommendations, 2021. Voir QRcode.
[30]Burkina Faso, Ivory Coast, Ufaransa, Madagascar, Quebec, Uswis, Tunisia, Vietnam na shirikisho la Wallonia-Brussels.
[31]Voir QRcode.

[32] Le livre en langue française en 2030 et 2050, Prospective economic study, Bearing Point. Voir QRcode.
[33]Voir QRcode.

Ripoti ya IOF
Lugha ya kifransa ulimwenguni katika mwaka wa 2022

Kamati : Nivine Khaled, Mkurugenzi wa lugha ya Kifaransa na tamaduni ya vikundi vya wanaozungumza Kifaransa (DLC).

Uratibu mkuu na uwasilishaji: Alexandre Wolff, Mkuu wa taasisis ya French Language Observatory.

Uratibu na marekebisho: Francine Quéméner, Mtaalamu wa Programu katika taasisi ya Observatoire de la langue française (ufunzi wa Kifaransa) na sera za lugha.

Uwasilishaji (DLC): Véronique Girard, Mtaalamu wa programu (kugunduliwa kwa maudhui ya kitamaduni); Aurélia Grosu, Mshauri (Lugha ya Kifaransa na wingilugha katika mashirika).

Ushirikiano: Mirana Andrianasy (mkufunzi); Pauline Hardouin (msaidizi wa programu katika taasisi ya Observatoire de la langue française).

Waliochangia moja kwa moja: Bernard Cerquiglini, Souleymane Bachir Diagne, Jean-Marie Klinkenberg, Richard Marcoux, Florence Mourlhon Dallies, Daniel Pimienta, Laurent Richard, Destiny Tchehouali, Rada Tirvassen.

Imetafsiriwa na Allan Aringo

Toleo hili ni muhtasari wa kitabu kinachoitwa
Lugha ya kifransa duniani katika mwaka 2022
Ilihaririwa na - mnamo Machi 2022.

(c) Éditions Gallimard, 2022.